KUCHUNGUZA DHAMIRA KATIKA NYIMBO ZA HARUSI KISIWANI UNGUJA: MIFANO KUTOKA NYIMBO TEULE

JINA ALI KOMBO

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SHARTI PEKEE LA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI- FASIHI) KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2019

UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayohusu "***Kuchunguza Dhamira katika nyimbo za Harusi Kisiwani Unguja: Mifano kutoka Nyimbo Teule*****"** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili (M.A Kiswahili- Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……

Prof. T. S. Y. M. Sengo

(Msimamizi)

Tarehe…….

HAKIMILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii, hairuhusiwi, kukaririwa, kuhifadhiwa, kubadilishwa, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha au kurikodiwa kwa utaratibu wowote katika hali yoyote bila ya idhini ya kimaandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, kwa niaba yake,

TAMKO

Mimi, **Jina Ali Kombo**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu binafsi, na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chengine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada nyengine yoyote.

Saini……

Tarehe ……

TABARUKU

Kazi yangu hii, ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa Mzee Ali Kombo Haji (Mzee Tindo Kombo), (Almarhum) Bibi Kama Makame Ali ambaye ameshatangulia mbele ya haki, Allah amlaze mahali pema peponi, Amina.

SHUKRANI

Kwanza, ninamshukuru sana Mwenyeezi Mungu (S.W), kwa kunijaalia afya njema iliyoniwezesha kufanya utafiti huu na kuukamilisha kwa salama. Ninapenda kutoa shukrani zangu kwa wasaidizi, Wahadhiri, Waelekezaji, pamoja na Wawezeshaji ambao wamechangia kukamilika kwa utafiti huu.

Shukrani zangu, maalumu ni za msimamizi wangu, Prof. T. S. Y. M. Sengo, kwa kuniongoza, kunishauri na kunihamasisha hadi kukamilika kwa utafiti huu. Mwenyeezi Mungu (S.W), Amjaalie afya njema. Ampe umri mrefu, Amzidishie imani, wema na upendo kwa wanafunzi wake.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru akina Prof. E. Mbogo, Dkt. Simpasa, Dkt. Maulid Haji Omar, Dkt Omar Adam kwa ushauri wao pamoja na miongozo yao, iliyosaidia kukamilisha kazi hii, Mwenyeezi Mungu, Awazidishie imani.

Shukrani za pekee, kwa wakuu wangu wa kazi, Bi Somoe Said Mussa na Mwalimu Suleiman Hamad kwa kushirikiana nami kwa kunistahamilia kipindi nilichokuwa katika kazi ya utafiti, kuniruhusu kufuatilia masomo yangu kila nilipohitajikana ndani na nnje ya sehemu yangu ya kazi. Mwenyeezi Mungu, Awazidishie imani na moyo wa huruma, Allah (S.W), Awalipe kila la kheri Duniani na kesho Akhera. Amina.

Shukrani maalumu zimuendee Mume wangu, Bw. Sadik Koke Kheir, kwa msaada wake wa hali na mali, na kunivumilia katika ulezi wa familia, kwa kipindi chote cha

masomo, pamoja na watoto wetu Mwenyeezi Mungu awazidishie upendo, uvumilivu na kufuata nyayo katika mema ya wazazi wao. Allah, Awape wepesi juu ya hayo.

Natoa shukrani zangu pia, kwa Walimu, Walezi walionipa elimu ya maarifa na elimu ya Mazingira tangu Msingi hadi kufikia hapa, pamoja na majirani wema, Allah Awape kila la kheri katika maisha yao, Duniani na Akhera Amina.

Shukrani za moyoni, zimwendee baba yangu mzazi, Mzee Tindo Kombo Haji ambaye alinistahamilia kwa kipindi kikubwa, ambacho tukawa, hatuonani, ila kunitakia kila la kheri kwa muda wote. Pia, sikuwasahau watunzi na waimbaji wa nyimbo za harusi

Bibi Chausiku Muhimu Pandu na wenziwe kwa mashirikiano yao mazuri Mwenyeezi Mungu Awazidishie upendo, Awape kila la kheri. Mwisho ninawashukuru wanafunzi wote wa Shahada ya Uzamili wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, na wale wote, ambao sikuwataja humu, kwa msaada wa kunishauri na kunielekeza, mpaka kazi hii ikawa hivi inavyoonekana. Ninathibitisha kwa dhati, kwamba kila mmoja amenipa mchango mkubwa sana, hii ni sawa na kujiwekea akiba na malipo yao watayakuta mbele kwa Mungu. Amin.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni Kuchunguza dhamira katika nyimbo za harusi Kisiwani Unguja ambapo malengo mahususi yalikuwa ni kuchambua dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya mjini na kuelezea uhalisia wa dhamira za nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari kwa jamii ya leo. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, usomaji makini na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa, nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya mjini zina dhamira mbalimbali ikiwa ni pamoja na masuala ya kupata watoto, kutoka nje ya ndoa, heshima baina ya wanandoa, kukosana kwa wanandoa, imani za kishirikina, uzuri wa mwanamke, mapenzi katika nyimbo za harusi na uwajibikaji. Dhamira zote hizi zimeonekana kuwa na uhalisia katika jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya mjini. Kupitia usaili tuliofanya nao ilibainika kuwa, dhamira zinazotajwa katika nyimbo za harusi zina uhalisia katika maisha ya leo ya jamii hiyo na kwamba nyimbo hizo zikizingatiwa na hadhira husika zinatoa mafunzo yenye madili kwa jamii.

YALIYOMO

UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI ii

HAKIMILIKI iii

TAMKO iv

TABARUKU v

SHUKRANI vi

IKISIRI viii

YALIYOMO ix

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti 1

1.2 Tatizo la Utafiti 4

1.3 Malengo ya Utafiti 5

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti 5

1.3.2 Malengo Mahususi 5

1.4 Maswali ya Utafiti 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti 6

1.6 Mipaka ya Utafiti 7

1.7 Mpangilio wa Tasinifu 8

SURA YA PILI:MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA 9

2.0 Utangulizi 9

2.1 Maana ya Nyimbo 9

2.2 Aina za Nyimbo 10

2.2.1 Nyimbo Bembelezi au Bembezi 11

2.2.2 Nyimbo za Tohara 11

2.2.3 Nyimbo za Kazi 12

2.2.4 Nyimbo za Mbolezi 13

2.2.5 Nyimbo za Harusi 14

2.3 Kazi Tangulizi kuhusu Nyimbo 15

2.4 Utafiti Tangulizi kuhusu Nyimbo za Harusi 17

2.5 Mkabala wa Kinadharia 19

2.5.1 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi 19

2.6 Hitimisho 23

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 25

3.0 Utangulizi 25

3.1 Eneo la Utafiti 25

3.2 Usanifu wa Utafiti 25

3.3 Kundi Lengwa 26

3.4 Sampuli na Usampulishaji 26

3.5 Aina ya Data zilizokusanywa 27

3.5.1 Data za Msingi 28

3.5.2 Data za Upili 28

3.6 Mbinu za Kukusanya Data 28

3.6.1 Usomaji Makini 28

3.6.2 Usaili 29

3.6.3 Upitiaji wa Nyaraka 30

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data 31

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo 31

3.8 Usahihi na Kuaminika kwa Data 31

3.9 Maadili ya Utafiti 32

3.10 Hitimisho 32

SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 34

4.0 Utangulizi 34

4.1 Uchambuzi wa Dhamira katika Nyimbo za Harusi 34

4.1.1 Suala la Kupata Watoto 34

4.1.2 Suala la Kutoka nje ya Ndoa 37

4.1.3 Kuheshimiana Baina ya Wanandoa 41

4.1.4 Kukosana Baina ya Wanandoa 44

4.1.5 Imani za Kishirikina 47

4.1.6 Uzuri wa Mwanamke 50

4.1.7 Mapenzi katika Nyimbo za Harusi 53

4.1.8 Uwajibikaji 58

4.2 Uhalisia wa Dhamira za Nyimbo za Harusi 61

4.2.1 Uhalisia wa Suala la Kupata watoto 61

4.2.2 Uhalisia katika Kutoka Nje ya Ndoa 63

4.2.3 Kuheshimiana baina ya Wanandoa 64

4.2.4 Kukosana Baina ya Wanandoa 65

4.2.5 Imani za Kishirikina 67

4.2.6 Uhalisia wa Uzuri wa Mwanamke 68

4.2.7 Uhalisia wa Mapenzi 69

4.2.8 Uhalisia katika Uwajibikaji 70

4.3 Hitimisho 71

SURA YA TANO: HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO 72

5.0 Muhtasari 72

5.1 Hitimisho 74

5.2 Mapendekezo 75

MAREJELEO 76

VIAMBATANISHI 80

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Nyimbo ni ni kipera cha utanzu wa ushairi ambacho kina historia ndefu katika maisha ya binadamu. Inasadikika kuwa nyimbo zilianza tangu pale binadamu alipoumbwa (Mungai, 2014). Kirumbi (1975) anaeleza kuwa nyimbo ni sanaa pana katika fasihi simulizi na huchukuwa nafasi kubwa katika maisha ya watu. Hii inajidhirisha pale ambapo ni vigumu kuona tukio lolote lile katika maisha ya binadamu linafanyika bila ya kufuatana na nyimbo. Kutokana na kila tukio la kijamii, kiuchumi, kisiasa au kiutamaduni kufuatana na nyimbo ndipo tunapopata aina mbalimbali za nyimbo. Aina hizo za nyimbo ni kama vile nyimbo za sifa, jando na unyago, mbolezo, bembelezi, nyimbo za siasa na nyimbo za harusi kuzitaja kwa uchache. Matteru (1983) anaeleza kuwa nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kuhusishwa na ngoma na pia kuchezwa na mwimbaji wake. Nyimbo hutekeleza jukumu maalumu. Nyimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii.

Mawazo haya kuhusu maana ya nyimbo ni muafaka kwani ni ukweli uliokuwa bayana kwamba nyimbo katika jamii hubeba majukumu maalumu yaliyokusudiwa na wanajamii kwa kufungamana na muktadha maalumu. Nyimbo za mbolezo mathalani huimbwa katika kipindi cha msiba na kufanya tukio zima la msiba kuwa na sura ya majonzi na huzuni. Si jambo la kawaida kuona nyimbo za msiba zikiimbwa katika shughuli kama vile za harusi au sherehe za kusimika viongozi. Hivi ndivyo namna nyimbo za zinavyofungamana na matukio na kuyafanya matukio husika kuwa na

uhalisia (Wamitila, 2003). Katika maisha ya jamii mbalimbali duniani nyimbo hutumika kama chombo cha kuelezea hisia na matarajio ya wanajamii katika mustakabali wa maisha yao (Yalwala, 1991). Pale inapotokea wananchi wanatamani kupata maendeleo ya aina fulani katika tasinia yoyote ile halafu hawaoni dalili ya kupata maendeleo hayo ndipo sasa wanapotunga nyimbo za kuelezea kusikitika kwao (Omari, 2009). Pia, pale wanapoona kuwa yale waliyoyatarajia yanafanikiwa hutunga na kuimba nyimbo zenye kusifu na kupongeza jitihada na mafanikio husika (Wamitila, 2008). Hii inaonyesha kuwa nyimbo ni chombo ambacho kinatumika kuwasilisha fikra na maoni ya wanajamii juu ya jambo lolote lile katika jamii yao. Itakuwa ni jambo la ajabu kuona katika jamii nyimbo zinachukuliwa kama kitu cha kujiburudishia tu na kusahau kuwa ni chombo maalumu cha kutoa elimu, maonyo, mafunzo, maadili na kuhimiza mtazamo chanya katika jamii.

Kimsingi, katika jamii kuna nyimbo ambazo huambatana na tukio la ndoa ambazo huitwa kuwa ni nyimbo za harusi. Harusi ni sherehe muhimu ya kitamaduni katika jamii mbalimbali duniani. Sherehe za harusi huambatana na kila aina ya tafrija zikiwepo nyimbo. Nyimbo hizi hutumiwa ktoa mawaidha na ujumbe kwa maarusi wapya, pamoja na matarajio ya jamii na majukumu ya maarusi pamoja na kuwasifu maarusi na wazazi wao (Mungai, 2014). Sherehe nyingi za harusi hufungamana na dini katika jamii zetu kitu ambacho hupambwa kwa nyimbo za harusi zenye mawaidha ya kidini. Kwa upande wa dini ya Kiislamu, sherehe za harusi huambatana na ntimbo za Kaswida huku zile za Kikiristo zikiambatana na nyimbo za Injili. Hii hutokea katika muktadha wa kidini lakini kuna muktadha wa kijamii ambao hufanyika mara baada ya kumalizika kwa itifaki za kidini. Katika muktadha huo

ambao sherehe hufanyika katika kumbi za sherehe au nyumbani huwa na nyimbo zake ambazo ni tofauti na zile za dini ingawa za dini pia zinaweza kupigwa katika muktadha wa nyumbani. Hii inathibitisha kuwa nyimbo hufungamana na muktadha maalumu. Jamii ya Watu wa Zanzibar huwa na nyimbo za harusi za kijamii ambazo ni tofauti za Kaswida lengo likiwa ni kuwapamba maarusi wapya ili kuipendezesha shughuli nzima (Ali, 2014). Jamii ya Wanzanzibari hutumia nyimbo za harusi kwa lengo la kuwaeleza maarusi juu ya masuala mbalimbali ya kiutamaduni na kijamii ambayo ni muhimu katika kustawisha ndoa na kujenga familia yenye kutambua wajibu wake. Katika nyimbo hizo za harusi wanajamii hufunzwa uwajibikaji, kudumisha mapenzi ya dhati na kuheshimiana ili kuleta maelewano baina ya wanandoa. Ali (2014) alifanya utafiti juu ya taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja na kugundua kuwa nyimbo ni kiungo muhimu katika kufanikisha shuguli ya harusi. Harusi ambayo hufanywa sambamba na utendaji wa nyimbo hutazamwa kama kitu kilichokamilika vizuri. Harusi ambayo hufanywa bila ya utendaji wa nyimbo huonekana kama kitu kilichopita tu bila ya kuwa na ukamilifu unaostahili. Hii ndio desturi ya Waswahili katika kisiwa cha Unguja na ukanda mzima wa pwani ya Afrika ya Mashariki.

Kwa hakika nyimbo za harusi katika muktadha wa shughuli ya ndoa ni kitu kinachothaminiwa sana katika jamii ya Waswahili. Baada ya kuliona hili tunaona kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa kuchunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibari. Tumeona pia ni vema tubainishe uhalisia wa dhamira hizo kwa jamii ya leo kwa lengo la kuona ni kwa namna gani dhamira za nyimbo hizo ni muafaka katika kusukuma mbele maadili, mafunzo na maarifa mbalimbali

kwa jamii yetu ya leo. Imekuwa ni jambo la kawaida kuona wanajamii wakifurahia nyimbo za harusi bila kuzingatia au kuelewa kile ambacho kinasemwa katika nyimbo hizo (Mungai, 2014). Hapa ndipo ilipotulazimu pia kuwa na sampuli ya watafitiwa ambao tulifanya nao usaili kuhusiana na nyimbo hizo kwa lengo la kushadadia hoja za utafiti huu. Hivyo, katika tasinifu hii tumechunguza dhamira za nyimbo za harusi katika jamii ya Wazanzibari na uhalisia wake kwa jamii ya leo.

1.2 Tatizo la Utafiti

Nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi ambacho kinafungamana na matukio ya kila siku katika jamii (Samwel, 2010). Tumeshuhudia katika jamii mbalimbali duniani kwamba nyimbo ndizo ambazo zimekuwa zikitumika katika kuchapusha kazi na kutoa elimu za aina anuai kwa jamii. Katika kipindi ambacho hakukuwa na utoaji wa elimu kwa njia za kileo za kuwa na darasa na mwalimu anafundisha, jamii iliweza kupata elimu kupitia nyimbo za aina mbalimbali. Nyimbo za harusi ni mojawapo kati ya aina ya nyimbo zilizofanya kazi hiyo (Ali, 2014). Wataalamu mbalimbali wamevutiwa katika kuchunguza nyimbo katika jamii za Waswahili na zisizokuwa za Waswahili kwa makusudio tofauti tofauti. Mungai (2014) aliangalia fani katika nyimbo za mtunzi Anastacia Mukabwa wa nchini Kenya. Nyimbo alizozitafiti ni za Injili lakini kimaudhui zinakaribiana sana na nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili. Hii ni kwa sababu nyimbo za harusi huimiza mambo mema mambo ambayo yanahimizwa pia katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari. Ali (2014) alitazama taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza fani zaidi kuliko wetu ambao unahusu dhamira ambazo ndizo huwasilishwa kutokana na matumizi ya fani.

Hivyo, utafiti wetu utaisaidia katika kupata upande mwingine wa dhamira zilizopo ndani ya nyimbo hizo za harusi na kuweza kuziba pengo la maarifa katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu moja na malengo mahususi mawili kama yanavyowasilishwa katika sehemu zinazifuata hapa chini.

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya Mjini.

1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni pamoja na:

i) Kuchambua dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya Mjini.

ii) Kuelezea uhalisia wa dhamira zilizopo katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya Mjini kwa jamii ya leo.

1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti huu ni pamoja na:

(i) Ni dhamira gani zinazojitokeza katika nyimbo za harusi za Wazanzibari wa wilaya ya Mjini?

(ii) Dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari wa wilaya ya Mjini zina uhalisia gani kwa jamii ya leo?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika jamii ya Wazanzibari na nyinginezo katika bara la Afrika na duniani kwa jumla kwa namna mbalimbali. Kwanza utafiti huu utasaidia kuziba pengo la maarifa ambalo limeachwa na watafiti watangulizi. Utafiti huu umehusisha nyimbo na pia data kutoka kwa watafitiwa kitu ambacho kinaufanya kuwa ni utafiti hai ambao umeibua masuala yaliyopo hivi sasa katika jamii. Tumeona kuwa ni vizuri tupate maoni kuhusiana na mtazamo wa wananchi kuhusiana na dhamira za nyimbo za harusi kwa nia ya kupata picha kamili juu ya mtazamo wao kuhusiana na nyimbo hizo.

Sambamba na hilo, utafiti huu una umuhimu mkubwa katika jamii kwani utasaidia katika kuongeza marejeleo katika utafiti juu ya nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili wa Wazanzibar. Marejeo katika taaluma ya nyimbo za harusi bado ni machache na kukamilika kwa utafiti huu kutasaida katika kuongeza idadi ya marejeleo ambayo yanaongeza chachu ya kufanyika kwa utafiti zaidi katika nyimbo za harusi. Watafiti wajao watakapoingia katika maktaba au katika mtandao na kukutana na utafiti huu wataelimika zaidi mara baada ya kuusoma na hapo hapo ndipo watakapogundua maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa utafiti zaidi.

Pia, kufanyika utafiti kuhusiana na nyimbo za harusi kutaifanya jamii ione kwamba nyimbo za harusi ni kitu muhimu ambacho wanatakwa kukienzi na kukithamini. Imetokea katika jamii baadhi ya watu kutopenda fani za fasihi ambazo ni za kwao na kupenda fani za kigeni ambazo zimeleywa na wageni au wanazisikia katika televisheni na mitandao ya kijamii. Kwa kutuona sisi tunachunguza nyimbo za harusi na kuwauliza maswali kadhaa tukiwa maskanini ni funzo tosha kwao kuona kwamba

nyimbo za harusi ni hazina muhimu katika jamii ambayo haipaswi kupuuziwa kwa namna yoyote ile iwayo. Wanajamii huwaamini sana wasomi na kila linalofanywa na wasomi hutazamwa kama jambo muhimu sana.

Utafiti huu pia ni muhimu sana katika kukuza nadharia ya kipera cha nyimbo katika utanzu wa ushairi. Nyimbo zinatajwa kuwepo katika dunia tangu tu pale binadamu alipoumbwa na kuanza kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha. Kufanyika kwa utafiti huu ni muhimu katika kuonyesha kwamba licha ya kuwa nyimbo zilianza tangu karne na karne lakini bado zina umuhimu mkubwa katika maisha ya leo ya jamii. Umuhimu wake upo katika kufunza, kuonya, kuadili, kujenga saikolojia ya binadamu kukabiliana na changamoto katika maisha ya kila siku.

Kwa upande wa nadharia za uhakiki wa fasihi, utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika kuonyesha ni namna gani nadharia ya Saikolojia changanuzi inavyoweza kutumika katika kuchambua dhamira katika nyimbo za harusi. Harusi ni sherehe zinazofanywa mara baada ya tukio la kufungwa kwa ndoa kukamilika. Hivyo ni shughuli ambayo inahusu moja kwa moja akili ya binadamu na kwamba nadharia Saikolojia inafaa sana katika kuchambua nyimbo za harusi. Hii itawafunza watafiti wajao nao kuitumia nadharia hii katika tafiti zao ambazo kwa namna moja au nyingine zinachunguza nyimbo katika muktadha kama wa utafiti huu.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar peke yake. Wazanzibari ni jamii ya Waswahili ambao kwa asilimia zaidi ya 95 ni waumini wa dini ya Kiislamu. Hivyo wana nyimbo ambazo hujulikana kama Kaswida ambazo huambatana na matukio mbalimbali ikiwemo

tukio la harusi. Pia, wanazo nyimbo nyingine za harusi ambazo hazifungamani na dini ingawa lengo la makundi haya mawili ni lilelile. Pamoja na kutambua kuwepo kwa makundi haya mawili ya nyimbo lakini sisi tumeshughulikia nyimbo za harusi ambazo si za kidini moja kwa moja ingawa athari za dini hazikosekani. Pia, katika nyimbo za harusi kuna masuala mbalimbali ambayo yanaweza kutafitiwa ikiwa ni pamoja na vipengele vya kimaudhui na fani. Sisi katika tasinifu hii tumeamua kushughulikia dhamira tu katika nyimbo hizo ili kuweza kutimiza lengo kuu la utafiti wetu. Dhamira ni moja kati ya vipengele vya maudhui huku vingine vikiwa ni falsafa, migogoro, ujumbe, mafunzo na msimamo wa mwandishi lakini sisi tumejikita katika kipengele kimoja tu cha dhamira. Hii imetusaidia kupata muda wa kutosha kutafiti dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo husika na pia kuelezea uhalisia wake katika jamii ya leo.

1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura tano zilizoandikwa na kuwasilisha masuala mbalimbali kwa namana ambayo inakubalika kiutafiti. Sura ya kwanza inahusu utangulizi ambao umehusisha usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Sura ya nne imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa namna ambayo imesadia kutimiza lengo kuu la utafiti huu. Sura ya tano imetoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia ambapo tumepitia kazi mbalimbali ambazo zinahusiana na mada ya utafiti. Lengo la kufanya mapitio ya kazi tangulizi ni ili kuona ni nini ambacho tayari kimeshaandikwa kuhusiana na mada ya utafiti. Hivyo, tumeona ni vizuri tuanze kwa kueleza maana ya nyimbo na kisha kufuatiwa na aina za nyimbo, kazi tangulizi kuhusu nyimbo na mwisho ni kazi tangulizi kuhusu nyimbo za harusi. Pia, katika sura hii tumewasilisha nadharia ya Saikolojia changanuzi ambayo ndiyo tuliyoitumia katika kuchambua data za utafiti wetu.

2.1 Maana ya Nyimbo

Nyimbo ni kipera katika utanzu wa ushairi huku vipera vingine vikiwa ni mashairi, tenzi, tendi, ngonjera, maghani na muziki (Njogu na Chimerah, 1999). Maana ya nyimbo imeelezwa na wataalamu mbalimbali akiwemo Matteru (1983) anayeeleza kuwa nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma au pia kwa kuchezwa na mwimbaji wake. Anaendelea kueleza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Maana hii ya nyimbo tunakubaliana nayo kwa sababu imeeleza pande mbili za namna nyimbo zinavyowasilishwa ambapo huweza kuwasilishwa bila ya muziki au sambamba na muziki. Mawazo haya juu ya maana ya nyimbo yanafanana na yale ya Njogu na Chimerah (1999) wanaosema kuwa wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana na ujumbe kwa jamii. Maana hii ya wimbo

imeongeza maneno kuwa ni lazima wimbo uwe na ujumbe kwa jamii husika na ikitokea kuna wimbo ambao unaimbwa lakini hauna maana yoyote basi huo hauwezi kuwa wimbo itakuwa ni kitu kingine kabisa. Wamitila (2003) anaeleza kuwa wimbo ni kile kinachoimbwa ambacho huwa na sifa anuai ambazo ni:

i. Sauti ya mwimbaji
ii. Ala au vyombo vya muziki (ingawa sio lazima)
iii. Matini au maneno yanayoimbwa
iv. Hadhira inayoimbiwa
v. Muktadha uliofungamana na wimbo huo kwa mfano ibada, sherehe, kilio na kadhalika.

Maelezo ya Wamitila (2003) kuhusu maana ya wimbo yameelezwa kwa kina zaidi kwa kuhusisha pia sifa za wimbo. Maelezo haya yametusaidia katika kuzifahamu vizuri nyimbo na hivyo kuwa rahisi kwetu kushughulikia nyimbo za harusi katika jamii ya watu wa Zanzibar. Naye M'ngaruthi (2008) anaeleza kuwa nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia na kwa mahadhi ya kupendeza. Maana hii ya wimbo inakaribiana sana na ile ya Wamitila (2003) ingawa hii haitaji sifa nyingi za nyimbo kama zile za Wamitila. Tunakubaliana naye kwamba ni kweli nyimbo ili ipendwe na hadhira ni lazima iwe imetiwa sauti nzuri ya kufutia na kupendeza.

2.2 Aina za Nyimbo

Nyimbo kama moja kati ya vipera vya utanzu wa ushairi zimegawanyika katika aina mbalimbali kila kundi au aina ikiwa na jukumu lake. Aina hizo za nyimbo zimewasilishwa katika sehemu inayofuata hapa chini.

2.2.1 Nyimbo Bembelezi au Bembezi

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa Bembelezi ni nyimbo ambazo huimbwa kwa lengo la kubembeleza watoto. Nyimbo hizi huimbwa kwa sauti laini na nyororo ambayo ni ya chini na huwa ni fupi sana. Maelezo haya tunakubaliana nayo kutokana na ukweli kwamba tumekuwa tukishuhudia nyimbo za aina hii katika mazingira yetu ya kila siku ambapo tunawaona wazazi hasa mama wakiwaimbia watoto wao kwa lengo la kuwabembeleza. Hata hivyo, nyimbo za watoto hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine. Aina hii ya nyimbo Bembelezi imetusaidia kufahamu kwamba nyimbo huimbwa kulingana na muktadha maalumu. Kwa sababu nyimbo hizi zimelengwa katika kubembeleza watoto basi hata sauti yake huwa ni nzuri na ya chini ambayo kweli inaweza kumliwaza mtoto na hata akalala usingizi. Katika nyimbo za harusi za jamii ya Watu wa Zanzibar tumechunguza dhamira na hivyo kufahamu kuwa nyimbo huwasilishwa kwa sauti za aina fulani zikiwa katika muktadha fulani kumetusaidia sana kuelewa dhamira katika nyimbo zilizoteuliwa.

2.2.2 Nyimbo za Tohara

Nyimbo za tohara ni aina ya nyimbo ambazo zinaimbwa katika jando na unyago kwa madhumuni maalumu (Wamitila, 2003). Jando ni taasisi ya kijamii ambayo hutumiwa kwa lengo la kuwafunza vijana wa kiume majukumu yao ya utu uzima na unyago ikiwa ni kwa ajili ya kutoa mafunzo kama hayo kwa vijana wa kike. Wamitila (ameshatajwa) anaeleza kuwa jando na unyago hufanywa kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i) Kuwajengea wahusika ujasiri

ii) Kukebehi wenye uoga

iii) Kuwapa moyo watahiriwa

iv) Kusisitiza majukumu yao

v) Kushangilia kuingia katika utu uzima

Maelezo ya Wamitila (2003) tunakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa kwani ni ukweli uliokuwa wazi kwamba nyimbo za tohara huimbwa kwa lengo la kuwajenga wahusika kisaikolojia kwamba wakubaliane na tendo la kutahiriwa na walione kuwa ni la kawaida. Nyimbo hizo huwafanya kuwa mashujaa ambao hawaogopi kitu na ndio maana katika jamii ya Maasai Morani anapotoka jandoni anakuwa yupo tayari kuweza kukabiliana na simba bila wasiwasi wowote. Maelezo haya yametoa mchango muhimu katika utafiti wetu ambapo tumeweza kutambua kuwa nyimbo huimbwa zikiwa na lengo maalumu na haziimbwi tu bila ya kuwa na malengo. Hivyo, tumeweza kubainisha ni kwa vipi nyimbo za harusi za jamii ya Watu wa Zanzibar zimesaidifu majukumu ya wahusika ambao ni maharusi na jamii kwa jumla.

2.2.3 Nyimbo za Kazi

Katika jamii mbalimbali nyimbo zimekuwa na mchango muhimu katika kuhakikisha kuwa kazi zinafanyika kwa ufanisi na tija. Nyimbo za kazi ni aina ya nyimbo ambazo huimbwa wakati kazi fulani inafanyika ili kuichapusha kazi hiyo iweze kumalizika kwa haraka na kwa ufanisi uliokusudiwa (Mulokozi, 1996). Itakumbukwa kuwa kutokana na teknolojia ya Kiafrika kuwa bado ni duni wakilima walitumia nyimbo ili kuwafanya wasichoke na kufanikiwa kulima sehemu kubwa ya shamba kwa siku. Sehemu kubwa ambayo ingelipaswa kulimwa kwa trekta lakini wao waliweza

kulima kwa mkono na kumaliza kwa muda mfupi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa nyimbo za kazi huwa sifa za:

i) Matumizi makubwa ya takriri

ii) Maneno mepesi yaliyo rahisi kujifunza na kuimba pale pale

iii) Kupokezana-kiongozi wa wimbo kupokezana wimbo na wenzake

iv) Madoido na vigelegele ili kufanya wimbo kuvutia

Maelezo haya tunakubaliana nayo kwani ni kweli katika nyimbo za kazi huwa kunakuwa na marudiorudio mengi ambayo huwekwa kwa makusudi ili kazi inayofanyika iweze kwenda sambamba na midundo au mapigo ya marudiorudio hayo. Mathalani, kama ni katika kilimo, hupendeza pale wanapoimba na kurudiarudia ndipo jembe nalo linanyanyuliwa juu na kushushwa chini ili kulima. Hii huwafanya waimbaji kulima kwa pamoja na hatimaye kufanikiwa kumaliza kulima ndani ya muda mfupi.

2.2.4 Nyimbo za Mbolezi

Mbolezi ni nyimbo ambazo zinaimbwa katika jamii pale kunapotokea msiba, janga au maafa fulani kama vile ajali ya gari, moto na kadhalika (Mulokozi, 1996). Nyimbo hizi huimbwa kwa sauti ya masikitiko ambayo huwa ni ya chini na huwafanya waimbaji wengi kutokwa na machozi wakati wanapoimba au kusikia watu wengine wakiimba. Nyimbo hizi haziimbwi katika muktadha ambao hauhusishi masuala ya msiba kwa sababu hufungamana na muktadha wake uliokusudiwa tu. Nyimbo hizi huimbwa na mwimbishaji na kisha kuitikiwa na waombolezaji. Mara nyingi nyimbo za mbolezi huhusisha maandiko matakatifu katika dini ikiwa ni

kuhuzunika kwa kumpoteza mmoja wa wanajamii lakini pia kuwakumbusha waombolezaji kuwa kifo kipo na kitamkuta kila mtu. Jambo la msingi na muhimu ni kila mtu kuhakikisha kuwa anatenda mambo mema ili aweze kuingia mahali pema peponi pale wakati wake wa kutengena na dunia utakapofika. Maelezo haya yametusaidia kutambua kwamba katika kipera cha nyimbo huwa pia kunahimizwa masuala ya dini na ibada.

2.2.5 Nyimbo za Harusi

Nyimbo za harusi huimba katika sherehe zinazoambatana na ndoa pale inapofungwa. Ndoa ni sherehe muhimu ya kitamaduni katika jamii zetu. Sherehe hii huandamana na kila aina ya tafrija zikiwepo nyimbo. Nyimbo hizi hutumiwa kutoa mawaidha ya ujumbe kwa maarusi wapya, pamoja na matarajio ya jamii na majukumu ya maarusi bila kusahau kuwasifu maarusi na wazazi wao. Maelezo haya ni sahihi kwani ili tukio la harusi litajwe kuwa limefana ni sharti liambatane na uimbwaji wa nyimbo mbalimbali. Si jambo la ajabu kuona katika jamii baadhi ya sherehe za harusi zinapofanyika kunakuwa na uimbaji wa nyimbo za taarab na muziki wa kizazi kipya al-maarufu Bongo fleva (Omari, 2009). Kimsingi, aina hii ya nyimbo ndiyo ambayo tumeitafiti katika utafiti wetu ambapo tumetazama dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar katika wilaya ya Mjini. Jambo la msingi lililotusukuma kufanya utafiti huu ni kutaka kufahamu ni dhamira gani zinazowasilishwa katika nyimbo teule za harusi.

Kwa jumla, tunasema kwamba zipo aina mbalimbali za nyimbo ambapo sisi tumeweza kuainisha aina tano ambazo tumezieleza kwa urefu. Aina hizo ni pamoja na nyimbo Bembelezi, nyimbo za tohara, nyimbo za kazi, nyimbo za mbolezi na

nyimbo za mbolezi. Aina nyingine za nyimbo ambazo hatujazieleza kwa kirefu ni nyimbo za mapenzi, nyimbo za kisiasa, nyimbo za tambiko, nyimbo za sifa, nyimbo za kumpa mtoto jina na nyimbo za dini. Nyimbo zote hizi huimbwa katika muktadha maalumu kwa lengo la kuwasilisha ujumbe maalumu. Hivyo, kufahamu kwetu aina mbalimbali za nyimbo kumetusaidia kupata uelewa mpana juu ya majukumu ya nyimbo katika jamii na kufanya utafiti wetu kuwa rahisi kukamilika.

2.3 Kazi Tangulizi kuhusu Nyimbo

Utafiti tangulizi kuhusu nyimbo umefanywa na wataalamu mbalimbali wakiwa na malengo tofautitofauti. Yalwala (1991) alifanya utafiti juu ya maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alibaini kuwa nyimbo hizo zinawasilisha maudhui mbalimbali kwa jamii. Miongoni mwa maudhui hayo ni kusisitiza upendo, amani, kuheshimiana, kusaidiana na kujaliana miongoni mwa wanajamii. Maudhui haya ndiyo pia yanayotarajiwa kuwasilishwa katika nyimbo teule za harusi za jamii ya Wazanzibar. Nyimbo za harusi kwa namna zinavyotungwa huwa zinakuwa zimechota mawazo katika mafundisho ya dini. Hivyo, utafiti wa Yalwala (ameshatajwa) umetusaidia sana katika kuziona dhamira katika nyimbo za harusi tulizozitafiti kwa urahisi na hatimaye kukamilisha uchambuzi wa data na hatimaye kuandika ripoti ya tasinifu hii.

Mulokozi (1996) aliandika kitabu ambacho kilihusu fasihi simulizi kwa ujumla wake na ndani yake kipera cha nyimbo kikaelezwa kwa mawanda mapana. Aina za nyimbo ambazo tumezieleza hapo juu kwa kiasi kikubwa zinatokana na kitabu hicho cha Mulokozi ambacho wataalamu mbalimbali wamekisoma na wao kuandika kwa maelezo yao. Kazi hii ya Mulokozi imeweka misingi ya kufanya utafiti zaidi katika

utanzu wa nyimbo ili kuona utajiri mkubwa wa dhamira zilizomo ndani ya nyimbo husika. Miongoni mwa aina za nyimbo alizozitaja ni pamoja na nyimbo za harusi ambazo ndizo tulizozitafiti katika tasinifu yetu. Hii imetupatia fursa ya kuchunguza dhamira zilizopo ndani ya nyimbo za harusi na pia kuona namna jamii inavyozipokea nyimbo hizo.

Mungai (2014) alifanya utafiti uliochunguza fani katika nyimbo teule za Anastacia Mukabwa huko nchini Kenya. Anamtaja mwimbaji huyu kama mwimbaji mwenye kipaji kikubwa cha kuimba nyimbo za Injili. Kipaji chake kinathibitika kupitia fani aliyoitumia katika nyimbo zake ambapo tunaelezwa kuwa ametumia wahusika, mandhari, toni, tamathali za semi, sitiari, ishara, umbo na mtindo. Japo utafiti huu ni tofauti na wetu lakini umetusaidia kutambua mchango wa fani katika kujenga dhamira katika kazi ya fasihi. Sisi tumechunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar ambapo kwa maarifa tuliyopata juu ya fani ya nyimbo ikawa ni kazi rahisi kwetu kuziona dhamira ndani ya nyimbo husika. Pia, mara nyingi nyimbo za Injili huwa na dhamira ambazo zinakaribiana na za nyimbo za harusi.

Naye Khalifa (2014) alifanya utafiti kuhusu masuala ya jinsia katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Katika utafiti wake alibaini kwamba mwanamke katika nyimbo hizo husawiriwa katika hali chanya na hasi ambapo hali hasi ndio huchukuwa nafasi kubwa zaidi. Amebainisha kuwa kwa upande wa hali hasi mwanamke anasawiriwa kama malaya, mbeya, mnafiki, laghai, mpenda fedha, asiyekuwa na mapenzi ya dhati na muuaji. Kwa upande wa hali chanya mwanamke anasawiriwa kama kiongozi mzuri, mvumilivu na mchapakazi. Kazi hii ingawa ni

tofauti na ya utafiti wetu lakini imejaribu kutuonyesha namna mwanamke alivyosawiriwa katika nyimbo husika kitu ambacho kinakaribiana sana na utafiti wetu. Katika utafiti wetu tumechunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar ambapo baadi ya masuala ya jinsia yaliyobainishwa katika utafiti wa Khalifa (ameshatajwa) pia tumeyaona katika utafiti wetu. Hivyo, utafiti huo ulituwezesha kupata uhakikika wa kile ambacho tulikuwa tunakifanya katika utafiti wetu.

Musembi (2016) alifanya utafiti juu ya mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za Jando katika jamii ya Wakamba. Katika utafiti wake amebainisha kuwa katika nyimbo za jando kumekuwa na mabadiliko makubwa ambapo hivi sasa vijana wanahimizwa zaidi katika kusoma ili kuweza kujitegemea katika maisha yao. Hapo awali, vijana walihimizwa sana katika masuala ya mahusiano na namna ya kutafuta mali kupitia ufugaji na kilimo bila ya kusisitiza juu ya elimu ambayo ndiyo itasaidia katika kuimarisha shughuli tajwa za uzalishaji mali. Haya ni mabadiliko muhimu katika maendeleo ya jamii ambayo hubadilika kila mara bila ya kumsubiri mtu. Maelezo haya yanaonyesha kuwa utafiti wa Musembi (ameshatajwa) umetusaidia kutambua kuwa maudhui ya nyimbo hubadilika kutoka kipindi kimoja na kingine. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu ambapo tumechunguza dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Wazanzibar.

2.4 Utafiti Tangulizi kuhusu Nyimbo za Harusi

Utafiti kuhusu nyimbo za harusi umefanywa lakini sio kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na nyimbo za muziki wa kizazi kipya ambao umepata umaarufu mkubwa katika miaka ya hivi karibuni. Ali (2014) aliandika tasinifu ya uzamivu juu

ya taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili kisiwahi Unguja. Katika utafiti huu alibaini kuwa nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Unguja zinasawiri sana masuala ya utamaduni wa Waswahili ambao umefungamana na mafunzo ya dini ya Kiislamu. Mafunzo hayo ni pamoja na kuwahimiza wanandoa kuhakikisha kwamba mara baada ya ndoa yao ni lazima wawe wanatekeleza ibada kwa kuzingatia taratibu zilizopangwa. Haya ni mafunzo ndani ya Quran tukufu lakini yamechukuliwa na kuwasilishwa kwa namna ya wimbo wa harusi. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwamba kuna uhusiano wa karibu sana baina ya dhamira za nyimbo za harusi na mafundisho ya dini. Katika utafiti wetu tumechunguza dhamira katika nyimbo za jamii ya Wazanzibari ambapo pia tulikuwa makini kutazama dhamira kwa jicho makini ili kuona kama zipo dhamira ambazo zina msingi wake katika mafundisho ya dini na kutolea maelezo stahiki.

Beyanga (2016) alifanya utafiti juu ya taswira ya ng’ombe katika nyimbo za harusi za jamii ya Washubi wa Karagwe mkoani Kagera nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa katika nyimbo hizo za harusi ng’ombe anasawiriwa kama alama ya ushujaa, uchapakazi, ukarimu, uzazi, uongozi na umiliki wa mali kutaja kwa uchache. Taswira hizi zimejengeka kutokana na faida mbalimbali zinazotokana na ng’ombe kitu kinachoonyesha kuwa katika jamii ya Washubi ng’ombe ni kitu muhimu sana. Mtafiti alibaini kuwa karibu katika kila wimbo wa harusi kunajitokeza taswira ya ng’ombe. Utafiti huu kwa hakika umetusaidia kupanua uelewa wetu juu ya namna dhamira zinavyoweza kuibuliwa kutoka katika nyimbo na hivyo kutufanya kuwa makini katika kuhakikisha kwamba kila neno lililotumika katika nyimbo teule za harusi tunalitazama kwa umakini zaidi. Hii ni

kwa sababu neno moja tu katika wimbo linaweza kuwa ndilo lililobeba dhamira fulani katika wimbo huo na maneno mengine kazi yake kushadadia dhamira husika. Baadhi ya dhamira tulizoziibua katika utafiti wetu zinafanana na dhamira zilizotokana na taswira ya ng'ombe katika nyimbo za harusi za jamii ya Washubi.

2.5 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia huelezwa kuwa ni muongozo, kanuni au tarabibu ambazo zinaelezea namna jambo au kitu kilivyo au kinavyotakiwa kuwa (Wamitila, 2002). Hakuna kitu au jambo katika maisha ya binadamu ambacho kinaweza kufanyika bila ya kuwa na muongozo kamili wa kufanyika kwa jambo hilo. Kwa mfano, ukizungumzia juu ya kuwa na mapenzi bora au mapenzi ya dhati katika jamii ni lazima mambo kadhaa yafanyike ndipo hilo liwezekane. Haiwezekani mapenzi ya dhati yakatoka upande mmoja tu na yakawa kweli ni mapenzi ya dhati. Mapenzi ya dhati ni sharti yatoke katika pande mbili za wapenzi. Huu ni mfano wa nadharia kuhusu mapenzi ya dhati katika jamii. Haiwezekani upande mmoja kwa mfano, mke akawa na mapenzi ya dhati kwa mumewe lakini mumewe akawa mtu mkorofi ambaye humpiga na kumtukana mkewe kila siku halafu kukawa na mapenzi ya dhati baina yao. Hili haliwezekani kabisa kwani mapenzi hayo yatafika mahali yakawa na ukomo. Hivyo, katika utafiti huu tumeiteua nadharia ya Saikolojia Changanuzi kwa sababu inahusiana moja kwa moja na masuala ya mapenzi ambayo ndio yaliyoshughulikiwa katika tasinifu hii.

2.5.1 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi

Saikolojia Changanuzi ni nadharia iliyoanzishwa na mtaalamu wa masuala ya Saikolojia anayefahamika kwa jina la Sigmund Freud katika karne ya 19. Mtaalamu

huyu alifanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na saikolojia ya binadamu na kufanikiwa kugundua masuala mbalimbali (Chapman, 2011). Anaeleza kuwa katika saikolojia ya binadamu kuna maeneo matatu ya ubongo ambayo ndiyo hufanya mwanadamu kufanya mambo mbalimbali ambayo anakuwa akiyafanya aidha kwa ufanisi au si kwa ufanisi. Maeneo hayo ni utambuzi (concious), utambuzi usio kamili (sub-concious) na kutojitambua (unconscious). Eneo la kwanza hili linahusika na utambuzi wa mambo ya kawaida ambayo yanahusika katika maisha ya kila siku ya mwanadamu kuhusu chakula, malazi, mavazi, elimu, dini na mambo mengine mengi (Sherwood, 2006). Haya ni mambo ambayo yanafanyika wazi na hakuna mtu ambaye anazuiwa au kuona aibu kuyafanya mambo haya kwa namna yoyote ile. Mtu kujitambua kwamba yeye ni mwanaume au ni mwanamke na hivyo anatakiwa afanye nini ni moja kati ya mambo yanayokaa katika eneo hilo la kwanza la ubongo au akili ya mwanadamu (Wamitila, 2002).

Eneo la pili la ubongo wa mwanadamu ni lile linajijulikana kuwa kujitambua kiasi ambapo hapa masuala ya ndoto na njozi huingia. Wanadamu huota na kupata njozi juu ya mambo mbalimbali ambayo kimsingi yanatokana na eneo la kwanza la ubongo wa binadamu. Mambo ambayo binadamu anayaota yanatokana na tafakari zake, shughuli zake na harakati zote za maisha ambazo amekuwa akizifanyia kazi kwa siku au hata masiku (Duck, 2007). Ni vigumu sana kwa mtu kuota kitu ambacho hajawahi kukifikiria katika maisha yake. Katika ulimwengu wa fasihi tunakutana na ndoto ambazo wahusika wanakuwa wakiota au kutamani maisha ya aina fulani. Shaaban Robert kwa mfano, ni mmoja kati ya watu ambao wamekuwa na ndoto kuwa siku moja duniani kutakuwa na mapenzi bora ambapo watu wote watapendana

na kuheshimiana. Machafuko ambayo yanatokea leo hapa duniani yanaweza kukomeshwa pale tu dunia itakapokuwa na mapenzi bora.

Eneo la tatu la ubongo wa mwanadamu ni lile la kutokujitambua ambapo unakuta mhusika anafanya jambo ambalo hajuwi kwa nini amelifanya. Hii ni kutokana na akili yake kuchanganyikiwa kutokana na mawazo au hali fulani ya maisha iliyomkumba wakati huo. Si jambo la ajabu kuona mtu ambaye hajuwi saa wala wakati na hata ukimuuliza unafanya nini hawezi kueleza hicho anachokifanya (Smart, 2007). Katika kazi za fasihi tunakutana na wahusika ambao kwa matendo yao wanaingia katika kundi hili. Moja kati ya mambo ambayo huwafanya watu kuwa katika hali kama hii ni masuala yanayohusiana na mapenzi. Mapenzi husababisha watu kuishi kwa kujitambua au kuishi bila ya kujitambua. Mtu ambaye amefanyiwa kitendo kibaya na mpenzi wake hupata mawazo mengi ambayo wakati mwingine humfanya kuishi bila ya kujitambua. Mathalani, mtu ambaye anaamua kujiua kwa kujinyonga kwa sababu mkewe au mumewe amemsaliti kwa kujihusisha na mapenzi na mtu mwingine ni mfano mzuri wa mtu aliyefanya tukio bila ya kujitambua. Kikundi cha watu fulani katika nchi kinapoamua kuipinga serikali iliyopo madarakani kwa kutumia njia ya vita pia ni miongoni mwa mifano inayoonesha kutokujitambua kwa watu hao. Kwani kama wangekuwa wanajitambua wasingelithubutu kufanya kitendo hicho ambacho wanajua kuwa kitasababisha mauaji ya raia wasiokuwa na hatia yoyote.

Mtaalamu huyu wa taaluma ya saikolojia anaendelea kueleza kuwa mwanadamu huongozwa na mambo makubwa matatu katika maisha ambayo ni mahitaji, wasiwasi na raha (Bouman, 2003). Mambo haya matatu ndiyo hukamilisha maisha ya

mwanadamu na kwa kiasi kikubwa mambo haya hujitokeza ndani ya yale maeneo matatu ya ubongo au akili ya mwanadamu tuliyoyaeleza hapo juu. Mahitaji ni yale mambo ya msingi kama chakula, malazi na mavazi ambapo binadamu akiyapata haya huweza kuishi maisha ya amani na utulivu. Kukosekana kwa mahitaji haya huweza kumfanya mwanadamu kupoteza sifa ya uanadamu wake na kuwa mnyama wa mwituni. Baadhi ya jamii huingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kutokana na kukosa mahitaji muhimu kuhusu maisha.

Jambo jingine ambalo linaongoza maisha ya binadamu ni kuwa na wasiwasi. Mwanadamu ni kiumbe ambaye kila mara anakuwa na wasiwasi kuhusu maisha yake hana uhakika nini kitatokea siku za usoni. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa na mamlaka ya uongozi katika jamii au mahali pa kazi lakini anakuwa na wasiwasi kwamba saa yoyote anaweza kunyang'anywa nafasi yake. Mara nyingi wasiwasi huo huweza kumfanya mtu huyo kufanya kazi yake kwa uadilifu ili asije akaharibu kazi yake. Lakini pia wapo ambao hushindwa kufanya kazi yao vizuri kwa sababu ya wasiwasi wa kuogopa kufanya baadhi ya mambo akidhani kuwa ataharibu. Katika kazi za fasihi kunajitokeza hali hizi pale ambapo wahusika wanakuwa na wasiwasi katika katika kutekeleza majukumu yao. Shaaban Robert kwa mfano, katika kazi zake nyingi anazungumzia juu ya kuwa na woga na wasiwasi kwamba ni moja kati ya tabia za binadamu na kuwa na tabia hizi ni moja kati ya mambo ya msingi ya kumfanya mwanadamu afanye vizuri katika maisha.

Jambo la tatu ambalo linaongoza maisha ya binadamu ni raha za aina mbalimbali huku raha kubwa kuliko zote ikiwa ni mapenzi hasa ya kingono. Freud anaeleza kuwa mtoto huanza kupata raha ya kujamiiana pale anaponyonya maziwa ya mama

yake kwa kupitia chuchu na mdomo wake (Smart, 2007). Mdomo wa mtoto huwa ni kama uke na chuchu za mama huwa ni kama uume. Hivyo, mtoto anaponyonya kutoka kwa mama yake huwa kama vile anajamiiana na hapo ndipo starehe ya kujamiiana hukuwa na kuendelea mpaka pale mtoto anapofikia umri wa ukubwa, yaani anabaleghe. Watoto wa kike huwa na mapenzi zaidi na baba na wale wa kiume huwa karibu na mama wakiamini kuwa ile raha ya kijinsia wataipata kutoka kwa wazazi wao wa jinsia tofauti na yao. Baada ya muda kupita, watoto hujitambua kwamba hawawezi kuwa na mahusisno ya kingono na wazazi wao na ndio hapo wanapoamua kutafuta wapenzi nje na nyumbani kwao. Wapo baadhi ya watoto ambao huwa hawaukubali ukweli huu na hivyo kuishia kuishi maisha ya bila kuwa na mpenzi.

Kimsingi, nadharia ya Saikolojia Changanuzi ni muafaka katika kuchambua dhamira katika nyimbo za kwa sababu mapenzi ni jambo la kisaikolojia. Nyimbo za harusi hueleza masula mbalimbali ambayo kwa namna moja au nyingine yanahusiana na akili ya binadamu. Jambo kubwa katika maisha ya ndoa ni mapenzi na hivyo kila kinachosisitizwa katika nyimbo hizo huwa ni mapenzi. Kwa mfano, kama dhamira katika nyimbo zinahusu uwajibikaji wa mke na mume katika familia yao basi ni dhahiri kuwa uwajibikaji huo utafanikiwa pale tu kunapokuwa na mapenzi ya dhati ndani yao. Mapenzi hayo ya dhati yatadhihirishwa kutokana na utambuzi wa kisaikolojia alionao kila mhusika baina ya mke na mume.

2.6 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia ambapo kwa jumla tumeona kuwa utafiti kuhusu nyimbo umefanyika kwa kiwango fulani

ambacho hatuwezi kusema kuwa ni kikubwa. Hata hivyo, kwa upande wa nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar hakuna utafiti uliochunguza dhamira katika nyimbo hizo. Hivyo, tumefanya utafiti huu na kufanikiwa kutimiza malengo ya utafiti ambayo yalielekeza kuchambua dhamira na kisha kuelezea uhalisia wa dhamira hizo katika jamii ya leo. Sura hii pia imewasilisha mkabala wa kinadharia ambapo tumetumia nadharia ya Saikolojia changanuzi katia kuchambua data za utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti ambazo tumezitumia katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wetu. Mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti kwani ndizo ambazo huwezesha kupatikana kwa data sahihi na zenye kuaminika. Hivyo, katika sura hii tumewasilisha vipengele vya eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data, mbinu za uchambuzi wa data, usahihi na kuaminika kwa data na maadili ya utafiti.

3.1 Eneo la Utafiti

Katika taaluma ya utafiti hakuna utafiti ambao hufanywa bila kumakinikia eneo maalumu ili iwe rahisi kukusanya data. Eneo la utafiti ni mahali ambapo data za utafiti zinapokusanywa kulingana na malengo mahususi ya utafiti husika (Kothari, 2008). Eneo la utafiti huu ni wilaya ya Mjini ambapo tumehusisha shehia za Chumbuni, Mlandege, Malindi, Bumbini, Bububu, Bait Al Ras na Darajani. Shehia hizi zilichaguliwa kutokana na kufanya harusi za mara kwa mara ambapo ilimwezesha mtafiti kukusanya data zake kwa urahisi. Pia, maeneo haya ya waimbaji maarufu wa nyimbo za harusi za kila aina na hivyo kuwa ni muafaka katika kumwezesha mtafiti kupata data za kutosha.

3.2 Usanifu wa Utafiti

Utafiti hufanywa kwa kuzingatia au kufuata mpangilio maalumu ambao husaidia kupatikana kwa data stahiki za utafiti. Mpangilio huo hujikana kama usanifu wa

utafiti ambao huelezwa kama ni ramani ambayo inaonyesha namna utafiti utakavyofanyika tangu katika kukusanya data mpaka kuzichambua na kuandika ripoti ya utafiti (Babbie, 1999). Utafiti huu umetumia usanifu wa uchunguzi kifani unaohusu kuteuliwa kwa eneo au jambo maalumu la kulifanyia utafiti. Katika utafiti huu tuliteua nyimbo za harusi za jamii ya Wanzanzibari wanaoishi katika maeneo ya Wilaya ya Mjini mkoa wa Mjini Magharibi. Tuliteua wilaya hii kwa sababu ni mjini na huwa kunafanyika harusi nyingi hivyo ikawa rahisi kwetu kuhudhuria harusi na kukusanya data. Mbinu hii imetusaidia kupata data za kutosha kuweza kujibu maswali ya utafiti wetu kwa gharama nafuu na muda mfupi. Mtafiti ni mkaazi wa wilaya hii hivyo hakupoteza muda mwingi kusafiri kwenda mbali kukusanya data za utafiti.

3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa ni wale ambao mtafiti amedhamiria kuwa ndio ambao watampatia data za utafiti wake (Young, 1984). Kundi lengwa huweza kuwa binadamu, wanyama, miti, fani ya fasihi na wadudu. Katika utafiti huu tulilenga kukusanya data kutoka kwa waimbaji wa nyimbo za harusi, wanandoa na wazazi katika jamii ya Wanzanzibari. Kundi hili limeteuliwa kwa sababu ndilo haswa linalohusika katika muktadha mzima wa kuhakikisha kuwa harusi inafanikiwa. Hivyo, tumeweza kupata muafaka za utafiti huu kutokana na kundi lengwa hili.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya watafitiwa ambayo huteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili kuwa ni kiwakilishi cha kundi zima (Robson, 2007; Creswell, 2009). Sampuli ya utafiti huteuliwa kwa sababu si kazi rahisi kwa mtafiti kuweza kukusanya data

kutoka kwa watu au watafitiwa wote ambao wanapatikana katika jamii. Hivyo, sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni watafitiwa 40 ambapo tuliteua waimbaji 10, wanandoa 15 na wazazi 15. Katika kila kundi tulizingatia jinsia na umri ili kuweza kupata data zenye mawazo ya kila kundi. Tuliamini kuwa waimbaji 10 wangeweza kutupatia nyimbo za kutosha kwa sababu kila mwimbaji ana nyimbo zaidi ya moja. Baada ya kusikiliza nyimbo zao tuliona kuwa zipo ambazo zinajirudia kwa wote na hapo ndipo ikawa tumehitimisha kuwa data tulizopata zinatosha. Wanandoa tuliwateua kwa sababu tulitaka kufahamu maoni yao juu ya nyimbo zilizokuwa zikiimbwa wakati wa harusi yao. Wazazi kwa upande wao, tuliwateua kwa lengo la kufahamu ni kwa vipi nyimbo zinazoimbwa katika harusi zinasaidia katika kuimarisha ndoa katika jamii ya Wanzanzibari.

Kimsingi, uteuzi wa sampuli hufanywa kwa kuzingatia utaratibu maalumu unaofahamika kama usampulishaji (Kumar, 1999). Katika kuteua sampuli ya utafiti huu tumetumia usampulishaji lengwa ambapo sampuli iliteuliwa kwa makusudi tukiamini kuwa itatupatia data tulizozihitaji katika utafiti wetu. Mbinu hii ya uteuzi wa sampuli ni nzuri kwa sababu humwezesha mtafiti kukusanya data zake kutoka kwa sampuli yenye uwezo wa kumpatia data za uhakika kuweza kutimiza malengo ya utafiti wake kwa muda na gharama nafuu (Yin, 1994).

3.5 Aina ya Data zilizokusanywa

Katika utafiti huu tumekusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili kama zilivyowasilishwa katika sehemu inayofuata.

3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni ghafi ambazo hazikuwahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa ajili ya kujibu maswali au kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika utafiti unaofanywa kwa mara ya kwanza kama huu wetu (Kombo na Tromph, 2006). Data za msingi hukusanywa kwa lengo la kuibua maarifa mapya ambayo hapo awali yaliwa hayafahamiki katika ulimwengu wa taaluma na kama yalikuwa yanafahamika basi ilikuwa ni kwa namna nyingine. Data hizi katika tasinifu hii zimekusanywa kutoka katika nyimbo za harusi zilizokusanywa kutoka kwa waimbaji walioteuliwa, wanandoa na wazazi katika jamii ya Wanzanzibari katika wilaya ya Mjini.

3.5.2 Data za Upili

Data za upili ni data ambazo tayari zipo katika machapisho na maandiko mbalimbali ya kitaaluma yaliyohifadhiwa katika maktaba. Data za aina hii hukusanywa kwa lengo la kujazilishia mawazo ya data za msingi ili kuweza kutoa ithibati ya baadhi ya mambo na kujenga mantiki. Data za upili katika utafiti huu tulizikusanya kutoka katika makala, tasinifu, majarida, vitabu, tovuti na wavuti.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini, usaili na upitiaji wa nyaraka kama zilivyowasilishwa katika sehemu inayofuata.

3.6.1 Usomaji Makini

Data za utafiti katika fani za fasihi kama vile nyimbo, mashairi, riwaya na tamthiliya hukusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kutoka kwenye maandishi ya kifasihi ambapo mtafiti pamoja na

msaidizi wake humakinikia maandishi husika na kuyasoma kwa makini na hatimaye kupata data za utafiti wake (Babbie, 1999). Mbinu hii tuliitumia katika kukusanya data kutoka kwenye nyimbo za harusi ambapo tulisoma nyimbo hizo kwa kurudia mara kadhaa mpaka tulipoona sasa tumepata data za kutosha. Ukusanyaji wa data kwa kutumia mbinu hii hufanywa kwa kuzingatia hatua ya kwanza ambayo kusoma nyimbo zaidi ya mara moja huku hatua ya pili ikiwa ni kudondoa sehemu ambazo zinaonekana kuwa zinahusiana na data husika. Hatua ya tatu ni kupangilia data husika katika mada ambazo zinaendana na malengo mahususi ya utafiti na hatua ya nne ni kuchambua data.

3.6.2 Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa mtafiti kufanya mahojiano ya moja kwa moja baina yake na watafitiwa (Kothari, 2008). Mtafiti huandaa maswali maalumu ya kumuongoza katika mahojiano ambapo huuliza mambo ambayo kwa njia moja au nyingine yanamsaidia kupata data za utafiti kulingana na malengo yake ya utafiti. Mbinu huu huwa katika aina mbili ambazo ni usaili funge na huru. Usaili funge ni ule ambao humpa mtafiti fursa ya kuuliza maswali ambayo tayari yana majibu na mtafitiwa hutakiwa kuchagua moja kati ya majibu yanayokusudiwa au yaliyokwishaandaliwa. Hii hutokea pale mtafitiwa anapoulizwa swali na kuambiwa ajibu “ndiyo au hapana.” Usaili huru, huu ni ule ambao mtafiti huuliza maswali ambayo hutoa uhuru kwa watafitiwa kutoa majibu kwa kujieleza kadri wanavyoweza. Mbinu hii ni nzuri kwa sababu inamsaidia mtafiti kupata data za kutosha kwa sababu kadri watafitiwa wanavyojieleza ndivyo mtafiti anaweza kupata data nyingine ambazo alikuwa hajakusudia kuzipata. Njia hii pia humwezesha mtafiti

kuuliza maswali ya ziada kulingana na namna mtafitiwa anavyojibu maswali na hatimaye kumsaidia mtafiti kupata data za kutosha na za uhakika zaidi. Mbinu hii pia ni nzuri kwa ajili ya watafitiwa ambao hawajuwi kusoma na kuandika kwa sababu wao wanazungumza tu hivyo ni rahisi kuwafikia watafitiwa wa aina hii.

Mbinu ya usaili katika utafiti huu ilitumika kukusanya data kutoka kwa waimbaji wa nyimbo za harusi, wanandoa na wazazi katika jamii ya Wanzanzibari katika eneo lililoteuliwa. Mbinu hii ilituwezesha kukusanya nyimbo 33 kutoka kwa waimbaji mbalimbali. Pia, mbinu hii ilitusaidia kukusanya data kutoka kwa wanandoa ambao ndio waliokuwa wakifanyiwa harusi pamoja wa wazazi katika eneo la utafiti.

3.6.3 Upitiaji wa Nyaraka

Nyaraka ni machapisho na maandiko ambayo yamehifadhiwa katika maktaba au makavazi kwa ajili ya kurejelewa na watafiti pamoja na wanafunzi wanaojifunza taaluma fulani. Hivyo, upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za utafiti hususani za upili kutoka katika makala, tasinifu, vitabu, magazeti, majarida, wavuti na tovuti ili kupata data za kutosha katika kushadadia hoja zilizojengwa na data za msingi (Yin, 1994). Utafiti wowote ule wa kitaaluma huwa tayari na utangulizi wake aidha wa moja kwa moja au wenye uhusiano wa karibu. Hivyo, ni vema kwa mtafiti kupitia nyaraka ili kupata taarifa tangulizi kuhusiana na kile anachokitafiti ili asije akajikuta anaeleza mambo ambayo yanatoka katika mantiki ya taaluma husika. Data za upili husaidia kujenga maoni ya mtafiti na kuwa yenye mantiki na kusaidia katika kutimizwa kwa lengo kuu la utafiti. Data za upili katika tasinifu hii zimekusanywa kutoka katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huchambuliwa kwa kutumia mbinu anuai kulingana na aina ya data zilizokusanywa kama ni za kimahesabu au kimaelezo. Data za utafiti huu ni za kimaelezo na hivyo zimechambuliwa kwa kutumia mbinu yam kabala wa kimaelezo.

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa kimaelezo kama unavyosomeka ni mbinu ya kuchambua data za utafiti kwa njia ya kimaelezo. Data za utafiti huchambuliwa kwa kutolewa maelezo ambayo husaidia kujibiwa kwa maswali ya utafiti bila ya kuhusisha mahesabu ya aina yoyote ile. Mbinu hii humpa mtafiti uwezo wa kuandaa mada ambazo anaona kuwa zinaendana na malengo mahususi ya utafiti wake na kisha kuzipatia data na kisha kuzichambua (Omary, 2015). Katika utafiti huu tulikusanya data ambazo zilikuwa katika mfumo wa kimaelezo na kisha kuzichambua kwa mkabala wa kimaelezo. Mtafiti alidondoa sehemu ya wimbo ambayo ilibeba data kulingana na mada au kichwa kilichoteuliwa na hatimaye kuchambua dondoo husika kwa kulitolea maelezo. Pia, tulinukuu baadhi ya maelezo ya watafitiwa tuliowafanyia usaili na kisha kuyachambua kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

3.8 Usahihi na Kuaminika kwa Data

Usahihi na kuaminika kwa data ndicho kitu ambacho kinafanya utafiti uweze kukubalika kuwa ni halali na unaweza kurejelewa kitaaluma na kitaalamu (Robson, 2007). Usahihi na kuaminika kwa data huweza kupatikana tu pale ambapo mbinu

sahihi za kukusanya data zinapotumika. Usahihi na kuaminika kwa data za utafiti huu umedhibitiwa na matumizi ya mbinu tatu za kukusanya data ambazo ni usomaji makini, usaili na upitiaji wa nyaraka. Mapungufu ya mbinu moja yaliweza kudhibitiwa na mabora ya mbinu nyingine na hatimaye kuweza kupata data muafaka za utafiti wetu. Data zilizokusanywa katika utafiti huu ni muafaka na zimeweza kutusaidia kuahakisha kuwa utafiti wetu ni imara na madhubuti.

3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti ni kipengele muhimu ambacho kinapaswa kuzingatiwa katika utafiti kwa lengo na kupata data muafaka kulingana na malengo ya utafiti. Maadili ya utafiti yalizingatiwa kikamilifu katika utafiti wetu ambapo tulitunza siri za watafitiwa wetu pale ilipotakikana kufanya hivyo ili kutokukika maadili ya utafiti. Tuliwasili watafitiwa ambao walikuwa tayari kutafitiwa na walioonyesha kutokuwa tayari tuliwaacha. Pia, tumewataja watafitiwa kwa majina yao ndani ya utafiti wetu baada ya kupata idhini kutoka kwao. Hivyo, maadili ya utafiti yamezingatiwa vizuri ndio maana tumeweza kukamilisha tasinifu hii kwa namna ilivyo.

3.10 Hitimisho

Mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wetu zimeteuliwa kwa umakini mkubwa ili kusadifu malengo mahususi ya utafiti. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini, usaili na upitiaji wa nyaraka. Mbinu hizi zimetusaidia kupata data stahiki kutokana na kwamba mapungufu ya mbinu moja yaliweza kudhibitiwa na mbinu nyingine na hivyo kupata data muafaka. Mbinu ya mkabala wa kimaelezo ndiyo ambayo imetumika katika

kuchambua data za utafiti huu ambapo maelezo madhubuti kulingana na malengo mahususi yametolewa katika sura ya nne ya tasinifu hii.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana na malengo mahususi ya utafiti huu ambayo yalikuwa mawili. Malengo hayo ni kuchambua dhamira katika nyimbo za harusi za Zanzibar na kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika nyimbo teule za harusi za Zanzibar. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumetimiza lengo kuu la utafiti ambalo ni kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo za harusi za Zanzibar.

4.1 Uchambuzi wa Dhamira katika Nyimbo za Harusi

Lengo mahususi la kwanza katika utafiti huu lilihusu kuchambua dhamira mbalimbali katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar na kwa kupitia nyimbo teule katika sehemu hii tumechambua dhamira hizo kama ifuatavyo:

4.1.1 Suala la Kupata Watoto

Suala la kupata watoto mara baada ya ndoa ni kitu ambacho kinatarajiwa na kila mtu katika jamii wakiwemo wana ndoa, wazazi wa pande zote, ndugu, jamaa na marafiki. Hii inatokana na ukweli kuwa pamoja na mambo mengine lengo kuu la ndoa ni kupata watoto ili kuendeleza kizazi (Sengo, 2009). Pale wana ndoa wanapopata mtoto au watoto wao binafsi huwa na furaha kubwa isiyokuwa na kifani. Pia, wazazi na ndugu wote wa pande zote mbili hufurahi sana na kufanya sherehe kumshukuru Mungu kwa kuwaongezea mwanafamilia mwingine. Hali inapokuwa ni kinyume cha matarajio na wanafamilia kuishi muda mrefu bila ya kupata mtoto wanandoa wenyewe huishi maisha ya taabu ya kutokuwa na maelewano baina yao. Baadhi ya

wanandoa huvumilia na kuwa na imani kuwa suala la kupata mtoto ni majaliwa ya Mungu na siku iliyopangwa na Mungu wao kupata mtoto ikifika basi watapata mtoto. Hata hivyo, ndugu hasa wa upande wa mume ndio huwa na kiranga cha kuona ndugu yao anapata mtoto na hivyo kumsema vibaya mke wa ndugu yao kuwa hana uwezo wa kupata mtoto na kwamba anakula bure tu kwa ndugu yao.

Kimsingi, suala la wanandoa kupata watoto mara tu baada ya kuoana ni jambo kubwa na linalotarajiwa na kila mtu. Mathalani katika nyimbo za harusi za Zanzibar kunajitokeza hali hii kupitia wimbo wa “Naiwe leo aee” kuwa:

> Na iwe leo aee, naiwe leo furaha
> Bibi amepata bwana, naiwe leo furaha
> Bwana amepata bibi, naiwe leo furaha
> Mtango nautambae, naiwe leo furaha
> Wende ndani ukazae, naiwe leo furaha
> Wazae mke na ndume, naiwe leo furaha
> Waje hapa tuwatume, naiwe leo furaha

Wimbo huu unaeleza bayana kuwa suala la wanandoa kupata mtoto muda mfupi baada ya ndoa ni jambo la muhimu sana na ni matarajio ya wanajamii. Hili tunalipata kupitia msitari unaosema, “Wazae mke na ndume,” ambapo inasisitizwa kuwa maharusi wazae watoto wa kike na kiume. Shangwe za nama hii ambazo zinakwenda sambamba na kauli kama hizi hujingia katika saikolojia ya wanandoa na wanajamii pia kiasi cha kuamini ya kuwa ni lazima maharusi hao watapata watoto. Hiki ndicho kitu ambacho kinawafanya maharusi kupata furaha kubwa pale wanaporuzukiwa mtoto aidha ni wa kiume au kike kwa sababu sasa saikolojia yao inakuwa imeshatulia tayari. Kupata mtoto katika jamii ya Waswahili ni riziki kubwa kutoka kwa Mungu ambayo humpasa aliyepata riziki hiyo kumshukuru Mungu kwa sala,

dua na kutoa sadaka. Tulipata fursa ya kufanya mahojiano na Mwanakombo Juma Fakih wa Chumbuni ambaye alitueleza kuwa:

> Kwetu sisi Waswahili tunajali sana uzazi na huwa tunakuwa na matarajio makubwa sana pale watoto wetu wanapoa kuwa watapata watoto. Hii ni kwa sababu watoto ndio ambao watarithi majina yetu na kuendeleza kizazi chetu. Sisi bibi na babu zao tunapoondoka duniani tunakuwa tumewaacha wao na hiyo inaashiria kwamba na sisi tunaendelea kuishi. Inapotokea kwamba maharusi wetu hajapata mtoto kwa muda mrefu huwa tunafanya ibada na dua maalumu za kumuomba Mungu awajaalie wampate mtoto. Pia, wapo baadhi ya wanajamii hutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwenda kwa waganga ili kupatiwa dawa za kuwawezesha kupata dawa (12/04/2017).

Nukuu hii inaonyesha kuwa suala la maharusi kupata watoto ni jambo muhimu sana katika jamii kiasi kwamba wazazi huingia katika ibada na pia katika kutafuta tiba mbalimbali kwa ajili ya maharusi wao kuweza kupata mtoto. Hapa ndipo tunapoona kuwa suala la maharusi kupata mtoto linaigusa saikolojia ya jamii nzima na sio la mtu mmoja mmoja. Katika mazingira kama haya wahusika ambao ni mme na mke huwa katika wakati mgumupale wanapotarajiwa kuwa wameshapata mtoto lakini unakuta bado mtoto hapatikani. Hali huwa mbaya zaidi pale wanapopata maneno kutoka huku na huko yakieleza sababu tofauti za kwa nini wao mpaka leo hawajapata watoto. Baadhi ya maneno hayo huwa hayashauri vizuri na kusababisha wanandoa hao kuachana au kujiingiza katika mambo mabaya ya kishirikina.

Saikolojia ya watu wengi katika jamii huamini kuwa mwanamke ndiye hasa anayetegemewa kwa kiasi kikubwa kukuza uzazi katika familia. Pale tu maharusi wanapooana na kukaa muda mrefu bila ya kupata mtoto mwanamke huwa ndiye mtu

anayelaumiwa kwa kiasi kikubwa. Hii ni kutokana na mtazamo wa jamii kuhusu mwanamke na uzazi. Katika wimbo wa “Alosema haolewi,” tunaelezwa ya kwamba:

> Alosema haolewi, hereni anazovishwa si za bure
> Mwambieni mwariwenu asikie, viatu anavyovishwa si vya bure
> Mwambieni mwari wenu asikie, na shanga anazovishwa si za bure
> Mwambieni mwari wenu asikie, na kanzu anayovishwa si ya bure
> Mwambieni mwari wenu asikie, na pete anayovishwa si ya bure

Wimbo huu unaonyesha bayana kuwa mwanamke ndiye anayetegemewa kuwa ataleta uzazi katika familia yake mpya mara baada ya kuolewa. Hili linabainika pale inapoelezwa kuwa ni vema mwari akaelezwa kuwa atambuwe kila anachopewa si cha bure bali anatakiwa akifanyie kazi kwelikweli na kazi yenyewe si nyingine bali kumpatia mumewe watoto. Tunasema hivi kwa sababu maneno kama haya huja mara baada ya muda kupita na wahusika kutopata mtoto na hutolewa na ndugu wa mume hasa wakike ambao ni mawifi wakidai kuwa mahari yao na vitu vingine virudishwe kwa sababu mke hazai. Hapa inaonyesha kuwa jamii bado haijaelewa vizuri suala la uzazi kuwa linawahusu watu wawili na upo uwezekano wa mume kuwa ndiye mwenye tatizo. Katika ulimwengu wa leo kuna vipimo vya aina mbalimbali ambavyo huonyesha tatizo lipo kwa nani baina ya mume na mke na hatimaye kulipatia ufumbuzi. Hivyo, si vema kwa watu kutoa lawama kwa mke kuwa ndiye mwenye tatizo la uzazi hata kabla ya kufanya vipimo na kubaini tatizo liko wapi. Umuhimu wa kufanya vipimo ni kwamba tatizo linaweza kugundulika na kuchukuliwa hatua za kimatibabu na kufanikiwa vizuri kwa wahusika kupata mtoto.

4.1.2 Suala la Kutoka nje ya Ndoa

Maisha ya ndoa yamezungukwa na mambo mengi likiwemo lile la mmoja au wanandoa wote kutoa nje ya ndoa zao. Tunapozungumza juu ya kutoka nje ya ndoa

tuna maana kuwa mke au mume anakuwa na mahusiano ya kimapenzi/kingono na mtu mwingine ambaye si mume wala mke wake. Hali kama hii husababishwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na tabia tu za wahusika (Sengo na Kiango, 2012). Katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar kunasawiriwa kuwa wapo wanandoa wanatoka nje ya ndoa zao kupitia wimbo wa "Babu Juma Kuchukuyu nini," kama ifuatavyo:

> Babu Juma kuchukuyu nini, kombe na vidagara
> Humo mkobani muna nini, rungu lina garagara

Mistari hii miwili ya shairi inaonyesha kuwa baadhi ya wanamume hutoka nje ya ndoa zao na kuwa na mahusiano ya kimapenzi na watoto wagodo. Matumizi ya neno "vidagara," katika msitari wa kwanza linarejelea mabinti wadogo. Hivyo, mume wa mtu ambaye ni mtu mzima anakuwa na mahusiano na watoto wadogo hali ya kuwa ana mke ndani ya nyumba. Wataalamu wa Saikolojia changanuzi wanasema kuwa, binadadamu ni kiumbe mweye tamaa sana na mara nyingi huishia kutamani watoto wadogo kimapenzi akiamini kuwa ndio ambao watamridhisha. Baadhi ya wanamume hujikuta wanakuwa na mahusiano baina yao na watoto wadogo ambao kimri wanaweza kuwazaa. Wapo pia baadhi ya wanawake ambao wanakuwa na mahusiano na vijana wadogo ambao wanajulikana kwa jina la "Serengeti Boys." Kwa hakika tabia ya tamaa za namna hii hazitakiwi kabisa katika jamii kwani huleta mathara mengi ikiwemo kuambukizwa magonjwa na kuwepo kwa wingi wa watoto wa mtaani. Kupitia wimbo huu unaoimbwa katika harusi, wanandoa na hadhara nzima ya harusi inaonywa kuwa si jambo la busara kuwa na mahusiano ya aina hii katika jamii. Heshima ya harusi ni kwamba wanandoa sasa watakuwa wamekuwa watu

wazima na ni wao wawili tu ndio ambao watakuwa na mahusiano ya kimapenzi kwa kuwa kuingia katika ndoa ndio maana yake hiyo.

Sambamba na hayo, pia suala la wanandoa kuwa na mahusiano nje ya ndoa linaendelea kusawiriwa katika nyimbo mbalimbali ukiwemo wimbo wa “Halina mana we Halina mana we.” Kupitia wimbo huu tunafahamishwa kuwa:

> Halina mana we halina mana we, Halina mana ntalikata x2
> La wenzangu linafuliwa pete, langu mie liko teketeke
> Halina mana ntalikata halina maana we, halina mana we mana ntalikata
> La wenzangu linatoa matunda, langu mie linatoa mafunza
> Halina maana ntalikata halina mana we, halina mana we
> halina mana ntalikata la wenzangu linatoa maraha,
> langu mie linaninyima raha…

Wimbo huu unaonyesha ya kuwa hakuna maelewano mazuri baina ya mke na mume na sababu kubwa inayotajwa hapa imeelezwa kwa lugha ya mafumbo. Nayo si nyingine ni kwamba tayari mume anaye au anao wanawake wengine nje ya ndoa. Hii ni kawaida inapotokea mume amepata mwanamke mwingine ambaye kisaikolojia anakuwa akiamini kuwa ndiye anayemridhisha kuliko mkewe wa ndani hujionyesha bayana kutokana na kule kutomheshimu mkewe. Tulifanya mazungumzo na Mzee Ali Mbwana Kombo wa Malindi kuhusiana na suala hili naye akatueleza ya kwamba:

Suala la uaminifu katika mambo ya ndoa limepungua sana katika kizazi cha leo. Hii inasababishwa na utandawazi ambapo bila aibu mwanamume ambaye ni mke wa mtu anaweza kuwa na mahusiano ya kingono nje ya ndoa yake. Kwa maoni yangu, ninaona hii ni tabia tu ambayo watu wanakuwa nayo kutokana na kuendekeza tamaa za kimwili. Wanawake ni watu ambao wamepewa elimu na Mungu ya kutambua mara moja kama mume ana mahusiano nje au la kutokana na mabadiliko ya ukaribu

wake na mume kuanza kubadilika. Mimi mwenyewe nimeshuhudia wanamume kadhaa wakiwa na mahusiano nje ya ndoa yao. Wanawake pia wenye mahusiano nje ya ndoa wapo na siku hizi wanaendelea kuongezeka kwa sababu ya tamaa ya vitu na fedha (24/05/2017).

Nukuu hii inatoa ushahidi kuwa suala la wanandoa kutoka nje ya ndoa lipo katika jamii na hivi sasa linaonekana kuwa ni jambo la kawaida. Hapo zamani ilikuwa ni vigumu sana kubaini kama mtu fulani ana mahusiano ya kimapenzi nje ya utaratibu kutokana na kufanywa kwa siri kubwa. Katika jamii ya leo usiri wa mambo haya umepungua sana na ni rahisi tu kumuona mume wa mtu akitoka katika chumba cha wageni ameongozana na mwanamke ambaye si mkewe. Katika wimbo hapo juu inaonyeshwa kuwa kila atakachofanya mke wa mtu kwa mumewe kitaonekana kuwa ni kibaya kwa sababu tayari mume anaye mwanamke mwingine ambaye ndiye anafanya mazuri zaidi. Hiki ni kitu kibaya na hakipaswi kuenziwa na jamii kwa sababu ni kinyume na maadili ya jamii na pia mafunzo ya dini. Wimbo huu unawataka wanajamii kujiepusha na mambo kama haya na bwana harusi pamoja na bibi harusi wanapaswa kuishi kwa kuzingatia maadili ya jamii na dini.

Wataalamu wa nadharia ya Saikolojia changanuzi wanaeleza ya kuwa hufika mahali wanandoa wakazoeana na mmoja wao akaona kuwa ni vizuri atafute mwenza nje ya ndoa. Mwanandoa wa aina hii huamini kuwa kila anachofanya ni kwa ajili ya kujiliwaza tu kwa muda na mkewe hawezi kufahamu suala hilo. Katika kufanya hivyo anajisahau na kunogewa na upande huo kiasi kwamba hata matumizi ya nyumbani hayapelekwi tena. Hapa sasa ndipo mke hubaini kuwa mumewe ana mahusiano na mwanamke mwingine. Wanawake wenye hekima na busara

huzungumza na waume zao au huyapeleka masuala hayo kwa wazazi ili yakajadiliwe. Baadhi ya wanawake wengine huchukuwa suala hilo kwa hasira na kuamua kufanya kisasi kwa yeye kuwa na mahusiano nje ya ndoa kama ilivyo kwa mume wake. Hizi zote ni saikolojia za wanadamu na kufanya hivyo huamini kuwa ndio suluhisho. Kwa bahati mbaya sana matokeo ya tabia hii ni kuleta magonjwa ya kuambukiza kama UKIMWI miongoni mwao na hatimaye kuishi maisha yenye shida na dhiki kubwa. Kama tayari wanandoa hao walikwishakuwa na watoto basi watoto wanaishia kuishi maisha ya taabu na wakati mwingine kuwa watato wa mtaani.

4.1.3 Kuheshimiana Baina ya Wanandoa

Suala la kuheshimiana baina ya wanandoa ni jambo la msingi sana katika kudumisha ndoa na pia katika kuleta hadhi ya ndoa katika jamii. Imezoeleka katika jamii kumtazama mwanamke kuwa ndiye mtu ambaye anatakiwa kumheshimu mume wake huku mume akiwa hatazamwi kwa jicho lile lile linalomtazama mwanamke katika suala la heshima. Hii inatokana na mfumo dume uliokuwa umetawala katika jamii ambao ulimtazama mwanamke kama mtoto mdogo ambaye anapaswa kumtii mume wake kwa kila kitu. Ni kweli suala la mwanamke kumheshimu mumewe ni muhimu lakini pia hata mume naye kumheshimu mkewe ni jambo la muhimu (Sengo, 1987; 1985 na 1992; Ramadhani, 2013). Katika nyimbo za harusi za Zanzibar tumeona dhamira hii ikisawiriwa katika wimbo wa “Kuna ila Moja ila yako Dada ila,” ambapo inaelezwa kuwa:

> Kuna ila moja ila yako dada ila, kutwa kwenda kwa mama ila
> Kuna ila moja ila yako dada ila, kitanda hutandiki ila
> …Kuna ila moja ila yako dada ila, mume umwite bwana ila

Dondoo hili linaonyesha kwamba mwanamke anapaswa kumheshimu mume wake na asimdharau kwa vyovyote vile iwavyo. Haya tunayapa katika maneno, “mume umwite bwana ila,” ikiwa na maana kuwa mke amtazame mume wake kama kiongozi ndani ya nyumba na kutii kila kitu anachaamriwa kukifanya. Matumizi ya neno, “ila,” yanaonyesha kuwa wanawake huwa wanajisahau katika kuwaheshimu waume zao na kuwatazama kama watu wa kawaida tu. Ndio maana katika wimbo huu wanaonywa kuwa sasa umeshaolewa na mume wako muite bwana na hata siku moja isijeikatokea tukasikia unamwita kwa jina lake. Kwa kufanya hivyo ndiyo ile dhana ya heshima kwa mume itajibainisha.

Jamii ya Waswaahili imepiga hatua kubwa katika kupunguza nguvu ya mfumo dume kwani hata mume naye anaelezwa kwamba ni wajibu wake kumheshimu mke wake ili kuifanya ndoa yao iwe ni ya furaha, upendo na amani. Haya tunayapata katika wimbo wa “Kuna ila moja ila,” kwamba:

> Kuna ila moja ila yako bwana ila, Kigongo mkononi ila
> Kuna ila moja ila yako bwana ila, mke kumwita bibi ila
> Kuna ila moja ila yako bwana ila, kula mkahawani
> Kuna ila moja ila yako bwana ila, kufanya na damu ila.

Wimbo huu unamtaka mume kumheshimu mkewe kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutompiga kwani itakuwa ni kumnyanyasa kijinisia. Pale anaposema, “kigongo mkononi,” ana maana ya kwamba si jambo la busara kumwadhibu mwanamke kwa kutumia fimbo. Baadhi ya wanamume wamekuwa wakiwaadhibu wake zao kwa kipigo kikali cha udhalilishaji mbele za watu jambo ambalo halikubaliki kabisa katika ulimwengu wa leo. Pale mke anapomkosea mumewe ni vizuri kumuonya kwa busara tena katika mazingira ambayo ni ya faragha ili kutomdhalilisha mbele za watu. Sambamba na hilo, pia mume anaelekezwa katika

wimbo huu kuwa ni wajibu wake kuhakikisha kwamba anamwita mkewe kwa heshima ya kuonyesha kweli huyu ni mkewe. Katika wimbo kunasemwa, “mke kumwita bibi,” kwamba ni vizuri kumwita mke kwa jina la heshima kuliko kumtaja jina lake au jina jingine ambalo sio zuri. Kumwita mke kwa jina zuri ni sehemu mojawapo ya kumheshimu.

Jambo jingine ambalo linatajwa kuwa ni la muhimu katika kumheshimu mke ni kula chakula alichopika na sio kula mkahawani. Pale mwanamume anapoanza tabia ya kula mkahawani na kuacha chakula kilichoandaliwa na mkewe inakuwa ni dharau kubwa sana kwa mke. Kula chakula kilichoandaliwa na mke ni moja kati ya vitu ambavyo vinawafanya wanandoa kuwa karibu na kudumisha mapenzi yao. Hii inakuwa ni rahisi wakati wa kula wanakuwa wanazungumza mambo mbalimbali kuhusu maisha yao na hatimaye kuimarisha mapenzi yao. Jambo jingine baya ambalo linaonyesha kutokumheshimu mwanamke kumlazimisha kufanya naye ngono wakati akiwa katika ada yake ya mwezi kwani humfanya mwanamke kujiona kwamba hathaminiwi kabisa na badala yake anachukuliwa kama chombo cha starehe tu kwa mwanamume. Kimsingi, inatakiwa mke aheshimiwe wakati wote hata kama si katika kipindi cha hedhi lakini akisema kuwa anaumwa au hajisikii vizuri kushiriki ngono basi hisia zake ziheshimiwe. Hii itamfanya kuwa mwenye amani na furaha wakati wote katika maisha yake.

Wataalamu wa nadharia ya Saikolojia changanuzi wanaeleza kuwa suala la ngono ni moja kati ya mahitaji muhimu katika maisha ya binadamu na kwamba pale mtu anapohitaji hutaka kutimiza azma yake kwa vyovyote vile iwavyo. Hata hivyo, ni lazima wanandoa wakajitahidi sana katika kujizuia pale mmoja wao anapokuwa

katika hali ambayo si mujarabu kwa tukio hilo. Ngono ni tukio la kisaikolojia na ni vizuri likadhibitiwa kisaikolojia. Pia, kuhusu mume kula mkahawani, wanasaikolojia wanasema kwamba mwanamke huwa katika lindi kubwa la mawazo swali kubwa likiwa ni kwa nini mume wake ale mahali kwingine. Tulipofanya usaili na Mwantumu Yusuf Kheir wa Mlandege alitueleza kuwa:

> Mimi kama mwanamke sipendi kabisa kuona mume wangu akila chakula mkahawani wakati mimi nimepika chakula nyumbani. Kitendo hiki kinaonyesha dharau kubwa kwangu kama mke kuwa pengine sijui kupika vizuri ndio maana anachukuwa uamuzi wa kwenda kula nje na nyumbani. Kama hilo ndio tatizo ni vizuri anieleze ili name nilijuwe kisha nijirekebishe ili niwe mpishi mzuri. Binadamu hakosi kasoro, inawezekana kabisa nikawa nakosea katika mapishi lakini nikiambiwa nitarekebisha na kufanya mambo kuwa mazuri ndani ya nyumba. Nitakuwa radhi na mume wangu kula nje ya nyumbani ikiwa ni katika shughuli na si vinginevyo (16/05/2017).

Maelezo katika dondoo hili yanaonyesha kwamba wanawake hawapendi kabisa tabia ya wanaume zao kula nje nyumbani kwao labda tu inapokuwa kwa jirani kuna kuna shughuli basi hapo tena hakuna namna ni lazima mume atakula shughulini. Shughuli tunayorejelea hapa ni harusi au msiba ambapo wahudhuriaji wote hupata fursa ya kula pamoja. Hivyo, wimbo huu unatoa funzo kwa mume kwamba alipochukuwa uamuzi wa kuoa maana yake tayari amekwishamaliza mambo ya kula mikahawani na sasa ale kile anachoandaliwa na mkewe.

4.1.4 Kukosana Baina ya Wanandoa

Binadamu ni watu ambao wanaongozwa na saikolojia yao katika kutenda au kutokutenda mambo mbalimbali katika maisha yao. Katika kutekeleza hilo, huweza kukwaza wengine au nao pia kukwazwa. Mume na mke ni watu ambao wanaishi kila siku mahali pamoja na hata kulala hulala pamoja. Hivyo, kukosana au kupishana

kauli ni jambo la kawaida kwao na hakuna mjadala juu yake. Maharusi katika sherehe ya harusi wanakumbushwa juu ya ukweli huu katika wimbo wa “Kero kero,” kwamba:

> Kero, keero we, kero kero we, kero kila siku
> Kwenda kwa wazazi we kero kero
> Uinamie chini we, uinamie chini x2
> Unapokwenda nyumbani kwa watu, uinamie chini.

Wimbo huu unaonyesha kuwa suala la kukosana baina ya wanandoa ni jambo la kawaida na ni vigumu sana kutotokea katika maisha ya kila siku ya jamii. Hata hivyo, kupitia wimbo huu maharusi wanaonywa kutokuendekeza mambo ambayo yatawasababisha wao kutoelewana na hatimaye kila siku wanakwenda kushitakiana kwa wazazi. Hili linaonekana pale mtunzi anaposema, “kwenda kwa wazazi we kero kero,” akiwa na maana kwamba mara nyingi kero baina ya wapenzi zinapozidi mmoja kati ya wanandoa hupeleka malalamiko yake kwa wazazi akishtaki kuwa mwenzake anamnyanyasa. Wazazi hulazimika kuitisha kikao cha usuluhishi kwa wanandoa husika. Mambo ya namna hii huchukuwa muda mwingi wa kazi kutokana na wakati mwingine kulazimika kusafiri kwenda kijijini kwa wazazi kwa lengo la kwenda kusuluhishwa. Hali kama hii haipaswi kupewa nafasi kubwa katika jamii kwani huchangia katika kurudisha nyuma maendeleo ya familia na taifa kwa jumla.

Katika wimbo huu pia kunaelezwa kwamba wanawake kutokana na silka yao ya umbeya huweza kusababisha kero baina yao na majirani kero ambayo inaweza kusababisha yeye na mumewe wakawa hawaelewani. Haya yanabainika katika kauli kuwa “unapokwenda nyumbani kwa watu, uinamie chini,” ikiwa na maana kuwa si jambo zuri kwa mke wa mtu kwenda kwa watu na kufanya kero ya aina yoyote ile.

Unapofika ugenini ni vizuri kuheshimu wenyeji au majirani ili kujiepusha na mambo mbalimbali.

Kimsingi, katika azma ile ile ya kuhakikisha kuwa wanandoa wanaishi kwa amani na kuvumiliana wakiwa na maelewano wimbo wa “Ukampare Samaki,” unathibitisha kwa kusema:

> Umetaka kuolewa, ukampare samaki
> Samaki ana magamba, ukampare samaki
> Samaki ana mwiba, ukampare samaki
> Samaki ana matumba, ukampare samaki

Wimbo huu ambao umewasilishwa kwa lugha ya mafumbo unaonyesha kuwa kuvumiliana katika ndoa ndio njia pekee ambayo itafanya jamii wanaondoa waendelee kuelewana katika maisha yao ya kila siku. Ikiwa mke atavumilia mapungufu ya mume wake ni wazi kwamba kutakuwa na maelewano baina yao kila siku na pale uvumilivu unapokosekana ni ukweli pia maelewano baina yao hayatakuwepo. Wimbo unaeleza kuwa pale mwanamke anapokubali kuingia katika ndoa hana budi kuwa mvumilivu ili ndoa yake iweze kudumu. Kitu kikubwa ambacho kinaweza kuifanya ndoa idumu ni maelewano baina ya mume na mke kama hakuna maelewano kila siku watajikuta wamepelekana kwa wazazi wakistakiana kwa mashitaka mbalimbali. Kauli kuwa, “samaki ana mwiba, ukampare samaki,” ni ishara ya kwamba ndani ya ndoa kuna mengi hivyo ni vizuri kuyavumilia.

Tulifanya usaili na mwimbaji wa wimbo huu anayejulikana kwa jina la Mwanamkuu Salim Pandu juu ya maana hasa ya wimbo huu naye akatueleza kwamba:

> Wimbo huu huimbwa kwa makusudi mazima ya kumjenga bibi harusi kisaikolojia ili ajitambuwe kuwa sasa yeye ni mtu mzima na nakwenda katika maisha ya ndoa. Yeye anayo tabia, maono, maadili yake na mwenzake pia anavyo vitu kama hivyo kwa upande wake. Sasa yeye kama mke anatakiwa alifahamu hili halafu ataekeleze majukumu yake kwa uvumilivu wa hali ya juu ili aweze kuwa na maelewano mazuri na mume wake. Mabinti wengi wa siku hizi hawana uvumilivu ikilinganishwa na sisi ndio maana ndoa nyingi hazina maelewano na masikizano kiasi kwamba haziwezi kudumu kwa muda mrefu kama ilivyokuwa kwetu mpaka leo tupo ndani ya ndoa zetu na uzee huu unaotuona nao. Hivyo, tunapoimba nyimbo kama hizi lengo letu ni kuhakikisha vijana wetu wanapata uelewa wa ugumu wa ndoa na namna ya kukabiliana nao (23/06/2017).

Nukuu hii inathibitisha kuwa ndani ya ndoa kunahitaji uvumilivu wa hali ya juu baina ya wanandoa ili kuifanya ndoa idumu kwa miaka mingi. Kutokana na athari ya mfumo dume tunaona kwamba anayetajwa kuwa anatakiwa kuwa na uvumilivu ni mke tu huku mume akiwa hatajwi mahali popote pale. Katika ulimwengu wa leo hata wanamume nao wanahitaji kuwa wavulivu ili kuleta maelewano ndani ya nyumba zao. Kama wanamume watakuwa ni watu wa hasira hasira tu ni dhahiri kwamba ndoa nyingi zitavunjika na hili tumeshaliona katika jamii yetu ambapo kila siku ndoa zinavunjika. Hii yote ni kwa sababu wanandoa wanakosa kuaminiana.

4.1.5 Imani za Kishirikina

Suala la imani za kishirikina lipo katika jamii nyingi duniani ikiwemo jamii ya Waswahili na Afrika kwa jumla. Imani za kishirikina hujitokeza pale mtu au kundi la watu linapoamini kuwa kuna watu ambao wana nguvu za giza za kuweza kufanya jambo fulani baya dhidi ya mtu au watu wengine. Mathalani katika wimbo wa “Masomaso we mwanangu usimuone,” kunasemwa:

Masomaso we mwanangu usimuone,
Masomaso we mwanangu usimuone
Kwa jicho la hasidi we mwanangu usimuone
Masomaso we mwanangu usimuone
Maso, mwanangu usimuone, maso, mwanangu usimuone

Wimbo huu unaeleza bayana kuwa wapo baadhi ya watu ambao ni washirikina na wanapomtaza tu bibi harusi basi hudhurika. Hivyo, kupitia wimbo huu washirikina wanatajwa bayana kuwa wapo katika harusi husika na washindwe kufanya chochote kibaya dhidi ya bibi harusi. Kisaikolojia mtu muovu anapotambuliwa na yeye kufahamu kuwa amekwisha fahamika huwa anakosa nguvu ya kufanya uovu wa aina yoyote. Hivi ndivyo saikolojia ilivyo pale muovu anapobainika hupatwa na bumbuwazi na kushindwa kufanya kitu chochote kibaya. Sambamba na hilo, wanasaikolojia changanuzi wanaeleza kuwa ni njambo la kawaida kwa binadamu wengi kutofurahia mafanikio ya watu wengine katika jamii. Suala la kuoa au kuolewa ni kitu ambacho hutazamwa kama mafanikio makubwa ya kimaisha kwa wanandoa jambo ambalo huwafanya baadhi ya watu kutofurahia mafanikio hayo na kuanza kufanya mambo ya ushirikina dhidi ya maharusi.

Katika namna hiyo hiyo ya kuendelea kuthibitisha kuwa suala la ushirikina lipo katika jamii wimbo wa “Leo ni leo ooo, Leo ni leo ooo,” unasema:

Leo ni leo ooo, leo ni leo ooo, utauona mpambano kweli si uongo
Jamani harusi mtoto wa watu, jamani harusi mtoto wa watu
Tumemzingua kwa Yasini tatu, tumemzingua kwa Yasini tatu
Asijedhurika, asijedhurika kwa macho ya watu, leo ni leo

Wimbo huu unaonyesha bayana kuwa suala la ushirikina lipo katika jamii ya Waswahili hususani katika shughuli za ndoa ambapo bibi harusi anatajwa kuwa

amepatiwa kinga dhidi ya watu wabaya ambao ni washirikina. Katika wimbo huu kuna msitari unaeleza, “tumemzingua kwa Yasin tatu, tumemzingua kwa Yasin tatu,” ikiwa ni dua ya kumkinga dhidi ya washirikina. Yasin ni moja kati ya sura katika Quran Tukufu ambayo husomwa kwa lengo la kuzuia aina yoyote ya ushirikina kumfikia mtu aliyesomewa. Hivyo, kitendo cha binti kusomewa Yasin tatu tayari kimeshampa kinga madhubuti dhidi ya maadui ambao ni washirikina. Tulipata fursa ya kumsaili shehe Noorden Shaban Khamis kuhusu maharusi kusomewa surat Yasin kama kinga dhidi ya washirikiana naye akatueleza ya kwamba:

> Yasin ni sura miongoni mwa sura za Quran ambayo ni kinga tosha dhidi ya kitu chochote kibaya ambacho imelengwa kimpate mtu au kundi la watu. Sisi mashehe huwa tunachukuliwa kwa ajili ya kwenda kuwaombea dua watu mbalimbali wakiwemo maharusi na huwa tunawasomea surat Yasini na Mungu hutoa ulinzi kwao katika kipindi chote kilichokusudiwa. Unajua tena katika harusi wanakuja watu wengi sana na kila mtu ana mambo yake wengine washirikina na wachawi na wengine mahasidi. Hivyo, kwa kumsomea bibi na bwana harusi surat Yasini inakuwa ni kinga tosha dhidi ya ubaya wowote ule (04/07/2017).

Maelezo ya mtafitiwa wetu hapo juu yanatoa ushahidi kwamba katika jamii kuna imani dhidi ya ushirikina kwamba upo na watu huchukuwa tahadhari yake. Kwa maoni ya wanasaikolojia wao wanaamini kuwa hili ni suala la saikolojia tu ambapo mtu anakuwa na imani fulani juu ya jambo wakati mwingine ni vigumu kuthibitisha kisayansi ukweli wa hicho anachokiamini. Hata hivyo, kile ambacho mtu anakiamini ndicho ambacho hutokea kwa sababu ni suala la kisaikolojia na kama tayari saikolojia yake imeshakubaliana na mtazamo kwa ushirikina upo na unafanya kazi daima ataiona nguvu ya ushirikina kwa sababu ni kitu ambacho kimeingia katika mawazo na fikra zake. Kwa maoni yetu tunaona kwamba ni jambo zuri kumuomba Mungu kwa lengo la kujilinda dhidi ya maovu pamoja na watu waovu. Hata hivyo,

haipendezi kumuona mtu akiwa ameshikamana sana na masuala ya ushirikina kwa sababu hayana tija yoyote zaidi ya kumpoteza mtu kisaikolojia akabaki akiamini mambo ambayo hayapo kabisa katika uhalisia.

4.1.6 Uzuri wa Mwanamke

Suala la uzuri wa mwanamke kuhusishwa na ndoa limepata mashiko sana katika jamii ambapo kila mtu anataka kuoa mwanamke ambaye ni mzuri kwa sura. Hufikia mahali hata waalikwa wa harusini hutoa sifa za uzuri wa mke wa mtu na wengine huanza kukosoa. Si jambo la ajabu kusikia watu waksema, “aisee bwana anajua kuchagua huyu kitu chake bombo kweli kweli,” na wengine utawasikia, “jamaa hamna kitu kabisa amekwenda kutuletea mtu ambaye sura wala shepu hana.” Maneno haya wanayasema utadhani wao ndio waoaji kumbe hawahusiki kabisa na muoaji ndiye aliyeridhika na uzuri wa mkewe yeye ndiye ambaye anaujua. Katika wimbo wa “Tumempata hatujampata,” ndiko ambapo tunaiona dhana ya uzuri wa manamke pale kunaposemwa:

> Tumempata hatujampata, tumempata mweupe kama mmanga
> Tumempata hatujampata, tumempata mweupe kama mmanga

Wimbo huu unaashiria kuwa mwanamke mzuri katika jamii ya Waswahili ni yule ambaye ni mweupe ambaye anakaribiana na Mwarabu. Hapa kuna matumizi ya tashibiha, “tumempata mweupe kama mmanga,” ambayo ndiyo yanathibitisha kwamba mwanamke mweupe ndiye hutazamwa kuwa ni mzuri katika jamii ya Waswahili. Hapa suala la tabia limewekwa pembeni ambapo ile tu mwanamke kuwa mweupe basi anakuwa ni mzuri. Jambo hili lina ukweli usiokuwa na shaka ndani yake kwani siku hizi vijana wengi huoa mwanamke kwa sababu tu ya uzuri wa rangi

yake na sura bila ya kuchunguza tabia yake. Hii husababisha ndoa nyingi kuvunjika baada ya muda mfupi tu tangu kufungwa kwa sababu tabia ya mke hufahamika tayari ndoa ikiwa imeshafungwa. Mzee Mohammed Sufian Nyange wa Mlandege alitueleza ya kwamba:

> Vijana wa siku hizi hawatazami tabia kama sifa ya msingi ya kupata mke bali wao hutazama sura na umbo la mwanamke. Hawafahamu kuwa sura na umbile la mwanamke ni vitu ambavyo vinachokwa ndani ya muda mfupi sana lakini tabia ndiyo ambayo hudumu katika maisha yote ya ndoa. Vijana wengi walioingia katika mkondo huu tayari walikwishatengana na wake zao kitambo. Hata hivyo, haina maana kusema kwamba, wanawake wote ambao ni wazuri kwa sura na umbo ni wana tabia mbaya la hasha! Wapo baadhi ambao mambo wana tabia nzuri na huwa na heshima sana kwa waume zao. Karibu harusi zote ambazo zimealikwa na kufanikiwa kuhudhuria ni chache sana ambazo zimeweza kudumu mpaka leo, nyingi zimevunjika ndani ya kipindi kifupi kabisa (17/05/2017).

Nukuu hii inakubaliana na mawazo ya wimbo kuwa vijana wengi wanapenda kuoa wanawake wazuri kwa sura na rangi kitu ambacho wakati mwingine huwagharimu sana. Kwa maoni yetu tunaona kwamba kitu ambacho kinawafanya wanawake wa aina hii wasiweze kudumu katika ndoa ni ile kutamaniwa na watu wengi kutokana na kuwa na maumbo ya kuvutia. Hii huwafanya kuwa na dharau kwa waume zao wakijidanganya kuwa hata kama akiachwa atapata mtu mwingine wa kumuoa. Jambo hili huwaumiza sana wanamume na kuishi maisha ya taabu na shida kubwa ya msongo wa mawazo na hatimaye kupata matatizo ya kisaikolojia. Mume hujikuta akijiuliza maswali mengi ya kwa nini mkewe amfanyie hivyo hali ya kuwa amemgharamia pesa nyingi na kila anachotaka anampatia. Maswali ya aina hii humfanya mume kuwa na mawazo mengi kiasi kwamba hata wakati mwingine anashindwa kujua afanya nini. Nukuu kutoka kwa Mzee Mohammed Sufian Nyange hapo juu inatoa fundisho kwa wanajamii wote kuwa makini wakati wa kuchagua

mke na itakuwa vizuri sifa ya tabia ya huyo anayekusudiwa kuwa mume ipewe kipaumbele halafu sifa nyingine ndiyo zifuate. Kama vijana wengi wakifanya hivi hakutakuwa na matatizo mengi ya ndoa kuvgunjika kama ilivyo hivi sasa.

Uzuri wa mwanamke unatokana na mambo mengi ambayo hufanywa na mwanamke mwenyewe pale anapoingia ndani ya nyumba. Kitendo cha mwanamke kujipamba vizuri na kujipaka manukato huweza kumfanya akawa mzuri sana hata kama hapo awali alionekana kuwa hana sura ya kuvutia. Katika wimbo wa “Kungwi mwambie mwari wako,” kunaelezwa ya kuwa:

> Kungwi mwambie mwari wako, asiache ufunguo
> Akiacha ufunguo, watafungua wenziwe
> Kungwi mwambie mwari wako, asiache kujipamba
> Asipojipamba, watajipamba wenziwe.

Dondoo la wimbo huu linasisitiza umuhimu wa mwanamke kujipamba kwa mumewe ili kumfanya aendelee kuwa mzuri kila siku mbele ya mamcho ya mumewe. Mwanamke anatakiwa kujipamba kwa ajili ya mumewe ili amuone kwamba ni mzuri kila siku na kamwe haipaswi kuona mwanamke amejipamba kwa ajili ya kujionyesha kwa watu wengine wa nje. Wimbo unaelekeza kuwa kama mke ataacha kujipamba basi uzuri wake hautadhihiri mbele ya mumewe na hatimaye upo uwezekano mkubwa wa mume kukmbia na kutafuta wanawake nje ya ndoa. Msitari mmoja wa wimbo hapo ju unasema, “asipojimba watajipamba wenziwe,” ikitoa maana kwamba suala la mwanamke kujipamba ni muhimu sana ili kumfanya asichokwe na mume wake. Kujipamba ni njia nzuri ya kumpatia mwanamke uzuri maridhawa akawa kama huyo ambaye anasifiwa kuwa ni mzuri tena mweupe kama mmanga. Kitu ambacho mwanamke hatakiwi kukifanya ni ile kujichubua mpaka ngozi inatoka

yenyewe ili eti awe mweupe kama Mwarabu. Jambo hili halikubaliki hata mara moja kwani linasababisha mwanamke kupatwa na matatizo ya saratani ya ngozi.

4.1.7 Mapenzi katika Nyimbo za Harusi

Mapenzi baina ya mke na mume ndio kitu ambacho kinatazamiwa baina ya mke na mume kwa sababu ndio kitu kilichowakutanisha. Maharusi wengi huoana mara baada ya kupendana ingawa hutokea mara chache watu kuoana bila ya kuoendana kwa dhati. Hii hutokea pale ambapo mwanamke anakuwa na mahusuaino ya kingono na mwanamume halafu kwa bahati mbaya anapata ujauzito wazazi wake humtaka aliyempa ujauzito huo kumuoa. Pia, katika jamii ya Waswahili hutokea mara kadhaa kuona kijana wa kike na kiume wakiwa na mahusiano kabla ya ndoa na mzazi wa kijana wa kike anapogundua huchukua hatua mara moja ya kumtaka kijana wa kiume kumuoa binti huyo. Jambo hili hutekelezwa kwa lazima hata kama kijana wa kiume alikuwa hajajipanga katika masuala ya ndoa. Katika nyimbo za harusi maharusi hufunzwa namna ya kuishi kwa mapenzi kama tunavyoona katika wimbo wa “Kuna ila moja ila,” kunaelezwa kwamba:

> Kuna ila moja ila yako bwana ila, kigongo mkononi ila
> Kuna ila moja ila yako bwana ila, mke kumwita bibi ila
> Kuna ila moja yako bwana ila, kuna mkahawani ila
> Kuna ila moja ila yako bwana ila, kufanya na damu ila

Dondoo la wimbo huu tulikwishalidondoa mahali fulani lakini hapa limetumika kusawiri dhamira ya mapenzi baina ya mke na mume. Mapenzi sio kupigana bali kuhurumiana ndio maana wimbo unasema, “kunai la moja yako bwana ila, kigongo mkononi ila,” ikiwa ni matumizi ya lugha ya ishara kuashiria kuwa watu ambao wanapendana siku zote hawawezi kupigana au mmoja kumpiga mwenzake.

Waswahili wanamsemo wao kuwa, “mwanamke hapigwi kwa fimbo bali kwa kipande cha kanga,” ambapo humtaka mume na mke kuishi kwa amani na upendo siku zote za maisha yao. Kumpiga mtu kwa kanga maana yake ni kutafuta maridhiano pale wawili wanapogombana na si kupigana. Hata hivyo, katika hali ambayo si ya kawaida ndoa nyingi ambazo zinakuwa zimefungwa kwa wahusika kulazimishwa huishia katika magomvi ya kila siku na ndio hao ambao wanashikiana vigongo. Wanasaikolojia wanakiri kwamba maisha ya ndoa ni kitu kigumu hasa inapotokea wahusika hawakuoana kwa dhati yao wenyewe bali kwa kulazimishwa. Ni vema kufahamu kwamba, kila mtu ana tabia yake na pale watu wawili wanapoama kuishi pamoja maana yake wanakuwa tayari wameshachunguzana tabia zao. Pale inapotokea wahusika wamefunga ndoa bila ya kuchunguzana tabia ni vigumu sana kuishi kwa mapenzi ya dhati katika ndoa yao. Hivyo, kupitia wimbo huu maharusi wanaelezwa kuwa ni vizuri kuishi kwa mapenzi bila kupigana kwani kupigana ni moja kati ya sifa zinazoonyesha kuwa hakuna mapenzi baina ya wawili hao.

Sambamba na hilo, ni sehemu ya mapenzi kwa wapenzi kuitana kwa majina mazuri ambayo ni maridhia kwa kila mtu baina yao. Pale mke anapoitwa “bibi,” hujisikia raha sana na kijuiona yeye ndiye yeye na hakuna mtu mwingine kama yeye hapa duniani. Hii humfanya kuwa na mapenzi ya dhati na mume wake na hatimaye ndoa yao kudumu milele hata milele mpaka pale watakapotenganishwa kwa kifo. Tulifanya usaili na bibi Mwanajuma Suleiman Shariff wa Chumbuni kuhusiana na masuala mbalimbali na katika hili akatueleza kuwa:

> Wanawake ni watu ambao wanapenda sana kuonyeshwa kuwa wao ni watu muhimu katika familia yao na kwamba bila wao mume ataishi maisha ya taabu. Ni wao wanawake ndio ambao wameshikilia furaha ya wanamume na hata wewe mwenyewe fanya utafiti wako utalibaini hili kwani pale ambapo kunakuwa na maelewano mabaya baina ya mke na mume daima huwa mwanamume ni mtu wa kuteseka sana akiishi maisha ya taabu na mashaka. Na pale ambapo mume na mke wanaelewana vizuri basi mume mara nyingi huwa na amani na furaha na hujituma zaidi katika kazi zake kwa sababu ana furaha ya roho. Hivyo, ni sifa ya mwanamke kuengwaengwa kwani humfanya kuwa na imani kwamba ni yeye tu na hakuna mwanamke mwingine nje ambaye anaweza kuchukuwa nafasi yake (30/05/2017).

Dondoo hili linathibitisha kuwa mapenzi ya dhati baina ya mke na mume ni muhimu sana kwani ndiyo ambayo huleta ustawi katika ndoa. Saikolojia ya mwanamke huridhika na kuamini kuwa hakuna ambaye anaweza kupendwa kama yeye pale ambapo mume anaonyesha kuwa kweli anampenda mkewe. Kumpenda huko ni rahisi tu kubainika hasa kupitia kumuita mke kwa majina mazuri na tena kwa kutumia lugha nzuri isiyokuwa ya ukali wala ukorofi. Hii humfanya mwanamke kuwa na amani ya roho na kujihakikishia mapenzi kutoka kwa mumewe nay eye binafsi kuendelea kufanya mambo mazuri kwa mume wake ili aendelee kupendwa. Hapa tunajifunza kuwa mapenzi ni suala la kisaikolojia na pale wawili wanapopendana basi vema kila mmoja akafahamu saikolojia ya mwenzake ili waweze kudumu ndani ya ndoa.

Kwa upande mwingine tunaonyeshwa kwamba mke naye anao wajibu wa kumuonyesha mume wake mapenzi ya dhati kwa kufanyia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumjali ili naye saikolojia yake iridhike kuwa hakuna mwanamume mwingine duniani kama yeye. Katika wimbo wa “Kungwi mwambie mwari wako,” tunapata mistari miwili ifuatayo:

…

Kungwi mwambie mwari wako amsinge mumewe,
Asipomsinga, atasingwa na wenziwe

Mistari hii miwili inaonyesha kuwa mwanamke anatakiwa kuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe kwa kumfanyia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumsinga. Kumsinga mume ni kitendo cha kumkanda mwili wake ili kuondoa machovu ya siku nzima. Kitendo hiki humfanya mume kuwa karibu na mkewe na kusaidia kudumisha mapenzi yao. Mwanamke ambaye atakuwa hana nafasi ya kumsinga mumewe basi atambuwe kuwa wapo wengi kule nje ambao watamsinga na hatimaye kumfutia kimapenzi na kuhamia kwao. Tunasema kitendo cha kumsinga mume kinawafanya wawili hao kuwa karibu kwa maana kwamba wakati huo kitendo cha kusinga kinaendelea wanapata fursa ya kuzungumza masuala mbalimbali kuhusiana na maisha yao. Imekuwa ni jambo gumu siku hizi mke na mume kupata wasaa wa kukaa muda mrefu pamoja kwa sababu kila mmoja anakuwa katika shughuli za kutafuta maisha ikiwa ni kazi au biashara. Mara nyingi hurudi nyumbani nyakati za usiku wakiwa wote wawili wamechoka na kuishia kulala. Sasa inapopatikana nafasi siku za mapumziko ya mwisho wa wiki ni vizuri kuyatumia kumsinga mume. Hapo ndipo fursa ya kuongea mambo mengi kuhusu maisha na familia kwa jumla itapatikana na hatimaye kudumisha mapenzi yao.

Vile vile, suala la mapenzi baina ya mke na mume linajidhihirisha katika nyimbo za harusi kupitia tendo la ndoa. Tendo la ndoa linatajwa kuwa ni moja kati ya vyanzo muhimu vya kudumisha mapenzi baina ya mke na mume. Mara nyingi mke na mume wanapokutana katika tendo la ndoa husahau tofauti zao na kufungua ukurasa mpya kabisa. Hili limebainika katika wimbo wa “Watoto lala,” ambapo kunaelezwa:

Watoto lala natakamkomoa baba yenu
Nikimpa robo ananuna
Nikimpa nusu ananuna
Natakampa yote nyama.

Wimbo huu unawasilisha dhamira ya mapenzi kwa lugha ya mafumbo ambapo mama anawataka watoto wake walale ili yeye apate fursa ya kufanya tendo la ndoa na baba yao. Inavyoonekana mke amebaini kuwa mapenzi yao yanashuka na ndio maana anaeleza kuwa sasa anataka kuhakikisha kuwa mapenzi yao yanaimarika kupitia tendo la ndoa. Wanasaikilojia wanaekeza kuwa, wanawake wengi huamini kuwa tendo la ndoa ndio silaha muhimu ya kudumisha mapenzi baina yao na waume zao. Huamini kuwa hata kama kulikuwa na ugomvi baina yao basi tendo la ndoa linatosha kumaliza ugomvi huo na kuwafanya kurudi katika hali ya kawaida ya mapenzi yao. Jambo hili lina ukweli ndani yake kwani hata wasuluhishi wa migogoro ya ndoa hujaribu kuwasihi wanandoa kukakaa pamoja ili kumaliza tofauti zao. Kukaa pamoja kunakosemwa hapa ni ndio huko kushiriki katika tendo la ndoa na kweli wengi hurejea katika mapenzi yao na kumaliza tofauti zao. Hata hivyo, wapo ambao ugomvi wao unakuwa tayari umekuwa mkubwa sana na huenda ni suala hilo hilo la tendo la ndoa ndilo lililowafarakanisha hivyo ni vigumu kuridhiana. Hii hutokea pale ambapo mume au mke amemfumania au amegundua kuwa mwenzake ana mahusiano nje ya ndoa kitu ambacho huwa vigumu sana kukisahau kwa wanandoa hao wanaposhiriki tendo la ndoa. Mara nyingi wanaposhiriki tendo la ndoa au kabla ya kushiriki hukumbuka kitendo hicho cha usaliti na hatimaye kukosa hamasa ya kushiriki katika tendo hilo la ndoa. Kwa jumla, wanandoa wanapewa elimu ya kwamba ni vizuri kuhakikisha kuwa kila mmoja anatimiza wajibu wake wa kuhakikisha kuwa anamtimizia mwenzi wake katika suala la tendo la ndoa ambalo

ndilo litawafanya kuendelea na mapenzi yao kwa miaka mingi mpaka pale Mwenyezi Mungu atakapomwita mmoja miongoni mwao.

Kupitia wimbo huu pia tunapata ufahamu kuwa katika suala la mapenzi hakuna mtu ambaye ni mmiliki wa tendo la ndoa kama ilivyokuwa inafahamika hapo zamani kuwa mume ndiye mmiliki wa tendo la ndoa. Hii ilitokana na mfumo dume uliokuwepo katika jamii ambapo mume ndiye aliyeamua saa na siku ya kufanya tendo hilo la ndoa na hata kama mke anahitaji tendo hilo hawezi kulipata mpaka pale mume atakapokuwa na nafasi. Mume aliweza kuoa wake wengi kiasi kwamba wengine walikaa muda mrefu bila ya kukutana na mume. Hata hivyo, katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni mfumo dume umepungua nguvu na katika wimbo hapo juu tunaonyeshwa kuwa mke naye sasa anaweza kumwambia mumewe anataka kufanya tendo la ndoa. Kitendo cha mama kuwataka watoto wake walale ili yeye apate fursa ya kushiriki tendo la ndoa na mume wake ni ishara kuwa mke naye ana sauti katika suala zima la tendo la ndoa. Wanasaikolojia wanaeleza kwamba kitendo cha kumfanya mke kutokuwa na maamuzi kuhusiana na tendo la ndoa kilifanywa kwa makusudi ili kumfanya mwanamke kuwa mtiifu kwa mume wake. Iliaminika kuwa kama mwanamke akiwa na sauti katika tendo hilo basi kuna wakati atamkatalia mume wake pale atakapomuhitaji. Hii ndiyo sababu kubwa ya kuifanya saikolojia ya mwanamke iamini kwamba ni mume tu ndiye mwenye maamuzi na suala hili.

4.1.8 Uwajibikaji

Dhamira ya uwajibikaji wa mke katika shughuli zake za nyumbani ni moja kati ya dhamira mardudi katika fasihi ya Kiswahili. Mke katika jamii hutazamwa kama mtu mwenye nafasi kubwa katika kuhakikisha familia na jamii kwa jumla inakuwa na

ustawi unakubalika. Mke ni mtu mwenye majukumu makubwa katika familia kiasi hata wanaharakati wa masuala ya jinsia kudai kwamba kumpa mwanamke majukumu yote hayo ni kumuonea na kumnyanyasa. Katika nyimbo za harusi mwanamke hukumbushwa wajibu wake huo kwamba anapofika nyumbani kwa mume ni wajibu wake kutimiza majukumu yake. Haya tunayapata kupitia wimbo wa "Kuna ila moja ila yako dada ila," kwamba:

> Kuna ila moja ila yako dada ila, kitanda hutandiki ila
> …
> Kuna ila moja ila yako dada ila, leo nimechoka ila

Mistari hii miwili inabainisha kuwa ni jukumu la mke kuhakisha kuwa kitanda chake kimetandikwa vizuri mara tu baada ya kuamka. Kitanda hapa kimetumika kisitiari kurejelea shughuli mbalimbali ambazo zinapaswa kufanywa na mke ndani ya nyumba. Kazi hizo ni pamoja na kusafisha nyumba yake, kuosha vyombo, kufua nguo, kupika chakula, kuwatunza watoto, kumtunza mume, kuwatunza ndugu wa upande wa mume na wale wa upande wake, kushughulikia masuala ya shamba na mifugo. Mke bora katika jamii hutazamwa kupitia uwezo wake wa kufanya shughuli hizi na kama ndio sifa ya muhimu ya kumfanya kuwa mke bora. Mwanamke ambaye ataonekana kutokuwa na uwezo wa kumudu shughuli hizi anahesabika kama si mke anayefaa na hivyo haolewi. Wanasaikolojia wanaeleza kuwa mwanamke yeyote yule tayari ameshajitambua kisaikolojia kuwa jukumu lake katika nyumba ni kuhakisha shughuli zote za ndani ya nyumba zinafanyika kwa wakati. Hivyo, mwanamke haitaji kukumbushwa juu ya wajibu huo kwani anajifunza kwa mama yake tangu akiwa mtoto.

Katika msitari mwingine wa wimbo hapo juu unaonyesha kuwa ni mwiko kwa mwanamke kudai kuwa amechoka. Anasema, “kuna ila moja ila yako dada ila, leo nimechoka ila,” kuashiria kuwa mwanamke wa aina hii ni mvivu hafai kabisa. Licha ya kuwa mwanamke ni mtu mwenye majukumu mengi ndani ya familia lakini haitakiwi hata mara moja kuonyesha kuwa amechoka. Mwanamke ni kiumbe ambaye hatarajiwi kuchoka kwa kuwa huaminiwa kuwa ni mtu mwenye nguvu za kutosha katika kutimiza majukumu yake kama mama. Hivyo, katika sherehe ya harusi bibi harusi anaelezwa kuwa asije akathubutu hata siku moja kudai kuwa eti amechoka katika kutimiza wajibu wake kwa sababu kwa asili mwanamke huwa hachoki katika kutimiza wajibu wake kama mke ndani ya familia. Kwa wanaufeministi wao wanaliona suala hili kama ni unyanyasaji dhidi ya jinsia ya kike kwa sababu mwanamke ni binadamu ambaye huchoka pale anapokuwa amejihusisha na shughuli mbalimbali za kila siku. Dhana hii imeshafahamika sana katika jamii kiasi kwamba siku hizi katika familia nyingi kuna wasaidizi wa kazi. Hii yote ni kwa ajili ya kumfanya mke asiwe na majukumu mengi ambayo ambayo yatamfanya achoke ashindwe kutimiza wajibu wake vizuri na kisha aonekane kama ni mtu asiye na uwezo wa kuitwa mke. Hata hivyo, wapo baadhi ya wanawake ambao ni wavivu katika kutimiza majukumu yao kiasi kwamba wanafanya kazi kidogo tu halafu wanasema kuwa wamechoka. Hii haikubaliki hata kidogo na ndiyo maana mwanamke anaonywa katika wimbo husika kuwa asisingizie kuchoka bali atimize wajibu wake kwa weledi mkubwa.

4.2 Uhalisia wa Dhamira za Nyimbo za Harusi

Nyimbo za harusi zilizotafitiwa ndani ya utafiti zimesheheni uhalisia kwa jamii ya leo kwa sababu kile kinachosemwa ndani ya nyimbo hizo kinatokea katika maisha halisia ya jamii. Nyimbo hizi hutazamwa kama chuo cha mafunzo ambacho wanandoa hupitia kwa lengo la kupata mafunzo ambayo watayatumia katika maisha yao. Kwa kiasi fulani wakati tunachambua dhamira tumegusia pia suala la uhalisia wa dhamira hizo japo kwa muhtasari. Hii ni kwa sababu ni vigumu sana kutenganisha uchambuzi wa dhamira na uhalisia wake kama ilivyo hata katika vipengele vya fani (Njogu na Chimerah, 1999). Hata hivyo tumeona kwamba ni busara katika sehemu hii tuelezea uhalisia wa kila dhamira ili kutimiza kikamilifu lengo mahususi la pili la utafiti wetu.

4.2.1 Uhalisia wa Suala la Kupata watoto

Kama tulivyoeleza mahali fulani katika tasinifu hii kuwa suala la kupata watoto mara baada ya ndoa kufungwa huwa ni matarajio ya watu waliowengi katika jamii ikiwa ni pamoja na wanandoa wenyewe. Wapo naadhi ya wanandoa ambao wanafanikiwa kupata watoto mapema lakini wengine wanachelewa kutokana na sababu mbalimbali za kiafya na kimaumbile. Wale ambao wanakosa kupata watoto baada ya muda fulani kupita ndio ambao wanapata matatizo ya kisaikolojia na kujikuta wanaingia katika imani za kshirikina. Tulipata fursa ya kuzungumza na maharusi katika harusi iliyofanyika katika eneo la darajani 13/04/2017 ambapo bwana na bibi harusi hao walitueleza ya kwamba:

> Sisi tunafuraha kubwa leo kutimiza shughuli hii kwa sababu tunaamini kwamba ni kwa majaliwa ya Mungu tumefika hapa. Si jambo jepesi kwa watu kuoana katika kipindi hiki kutokana na sababu mbalimbali lakini sisi tumevuka, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. Jamobo pekee ambalo sasa tunalitegemea ni kwamba Mwenyezi Mungu atatujaalia kupata watoto wema muda mfupi ujao ili tuwe tumetimiza azma yetu ya kuwa na familia bora.

Nukuu hii inaonyesha kuwa suala la kupata watoto ni suala lenye uhalisia katika jamii ambapo kila mwanandoa anapenda kupata watoto muda mfupi tu mara baada ya ndoa yake kufanyika. Katika mazingira kama haya ni vigumu sana kukubaliana na hali pale wahusika wanapochelewa katika kupata mtoto. Hata hivyo, jitihada nyingi hufanyika ili kuhakikisha kuwa watoto wanapatikana. Jitihada hizo huhusisha kutumia rasilimali mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha katika kutafuta tiba kwa waganga wa tiba za hospitali na tiba asilia. Pale inapotokea hakuna mwelekeo wa kupatikana kwa watoto wanandoa huingia katika mgogoro unaosababishwa na saikolojia zao kutokubaliana na hali hiyo. Hivyo, ni vema kwa wanandoa kusikiliza ushauri wa madaktari pale inapoonekana kuwa kuna shida fulani ya kiafya ili ipatiwe ufumbuzi na kama hakuna ufumbuzi basi pia ni vizuri kukubaliana na hali halisi kuhusiana na suala la wao kupata mtoto. Ipo mifano hai ya watu katika jamii ambao walikuwa na maisha mazuri wakiweza kumudu vizuri gharama zote za maisha. Lakini mara baada ya kushindikana kupatikana mtoto wamechanganyikiwa kisaikolojia na kuishia kuuza kila kitu ili wapate mtoto bila mafanikio na sasa ni maskini wa kusaidiwa. Wengine wamekuwa vichaa kabisa ambao hawawezi tena kupambanua jema na baya. Yote hii ni kwa sababu tu ya kukosa mtoto.

4.2.2 Uhalisia katika Kutoka Nje ya Ndoa

Suala la wanandoa kutoka nje ya ndoa ikiwa na maana kwamba wanakuwa na mahusiano nje ya ndoa zao ni jambo ambalo lipo kiuhalisia katika jamii. Hii inathibitishwa pia na takwimu za maambukizi ya UKIMWI ambazo zinaeleza kuwa miongoni mwa watu walioambukizwa virusi hivyo ni wandoa kwa idadi kubwa ikilinganishwa na wale ambao bado hawajaingia kwenye ndoa. Hii ni dalili tosha ya kuonyesha kwamba suala la wanandoa kutoka nje ya ndoa lipo wazi kabisa. Katika maisha halisia ya jamii kuna msemo kuwa “mume si wa mtu mmoja na mke si wa mume mmoja,” msemo ambao unathibitishwa kwa vitendo na wengi kati ya wanajamii. Wanasaikolojia changanuzi wanaeleza kuwa binadamu ni mtu ambaye ameumbwa na kuwa na sifa ya tamaa ya kutoridhika na kile alichonacho. Ni mtu ambaye ndani ya muda mfupi huchoka kitu na kutaka kubadilisha akiamini kwamba kingine ni kizuri kuliko kile cha mwanzo. Hii hujijenga na kuwa ndio tabia na hapo sasa inakuwa ni vigumu kuiacha. Tulizungumza na bwana mmoja ambaye hakupenda jina lake kudhihirishwa akatueleza ya kwamba:

> Kwa kweli suala la kutoka nje ya ndoa lipo sana katika kizazi chetu sisi kuliko hata ilivyokuwa huo zamani. Ninasema hivi kwa sababu zamani wazazi wetu waliweza kujizuia kwa sababu wanawake walikuwa wanajisitiri vizuri kiasi kwamba haikuwa rahisi kumtamani mwanamke kama ilivyo hivi sasa. Hebu we tazama tu yule mwanamke anayepita pale (kulikuwa na mwanamke anapita malindi kuelekea bandarini) amevaa nguo fupi, inayombana na kuonyesha mapaja yake yakiwa wazi. Katika hali kama hii wewe unataraji nini? Katika maadili ya hapa Zanzibar ilikuwa si jambo la kawaida kuona maumbile ya mwanamke kama hivi, jambo ambalo sasa linawashawishi wengi kujiingiza katika zinaa. Wanamume ambao tayari wamekwishaoa wanapoona mwanamke wa aina hii hutamani kufanya naye mapenzi akiamini kuwa ni mzuri kuliko mke wake aliyepo nyumbani (18/05/2017).

Nukuu hii inatoa picha kamili inayoonyesha kuwa suala la wanandoa kutoka nje ya ndoa ni jambo ambalo hivi sasa limekuwa ni la kawaida kutokana na utandawazi ambao upo katika jamii. Jamii inapaswa kufahamu kuwa kudumu na mke mmoja bila ya kutoka nje ya ndoa ni njia nzuri na muafaka ya kujiepusha na magonjwa kama UKIMWI ambayo ni hatari sana katika ustawi wa familia. Wanawake nao wasikubali kuwa na mahusiano nje ya ndoa kwa sababu ya tamaa za ajabu ajabu ikiwa ni pamoja na kudanganywa kwa fedha na vyakula kama chipsi kuku au chipsi mayai. Wakati wanafikria kufanya mambo haya wakumbuke juu ya hatma ya uhai wao, waume zao na ustawi wa familia kwa jumla.

4.2.3 Kuheshimiana baina ya Wanandoa

Kuheshimiana baina ya wanandoa ni jambo la msingi mno katika jamii na pale wanandoa wanapoheshimiana daima huwapo na maendeleo. Kuheshimiana kama tulivyokwisha kueleza hapo awali ni ile hali ya kila mmoja kumjali na kumthamini mwenzi wake kwa namna ile ile ambayo yeye binafsi angepaswa kuheshimiwa. Suala la kuheshimiana katika jamii lina uhalisia katika jamii ambapo siku hizi kutokana na wanandoa wengi kuwa wote ni wafanyakazi na wengine ni wafanyabiashara. Hii inatokana na kwamba wote wawili wanamchango muhimu katika kukuza pato la familia hivyo kunakuwepo na kuheshimiana. Tulizunguza na Rayya Makame Fakih wa Mji Mkongwe tuliyekutana naye katika eneo la Forodhani na kutueleza kuwa:

> Siku hizi katika majumba yetu waume na wake tunaheshimiana sana kwa sababu ule utegemezi kwa mume kwa kila kitu umepunga ati. Kwa mfano kama mimi ni mwalimu wa skuli ya msingi leo nimekuja hapa na familia yangu akiwemo mume wangu na mimi ndiye mlipaji wa kila kitu. Nimemwambia mume wangu kuwa leo ninaitoa familia yangu yote outing na akakubali na ndio unatuona tuko sote hapa. Hii inasaidia sana kujenga heshima baina yetu kwa sababu hata mume wangu anaona mchango wangu katika maendeleo ya familia yetu. Hili unaliona leo la outingi ni moja tu lakini tunasaidiana katika mambo mengi mimi na mume wangu katika kusomesha watoto tena na mambo ya ujenzi ambapo hapa tunapoongea tunaishi kwenye nyumba yetu binafsi tuliyojenga kwa pamoja na mme wangu (22/05/2017).

Nukuu hii inaonyesha kwamba heshima baina ya wanadoa huja pale ambapo wote wawili wanasaidiana katika kuendesha maisha yao. Inapotokea mwanamke anasaidiana na mume wake katika gharama za maisha hapo ndipo heshima inapopatikana. Jambo hilini la kweli kwani pale mwanamke anapokuwa na mchango katika kuendesha maisha hata mume humuheshimu sana mkewe ikiwa ni pamoja na kusikiliza maoni ya mkewe juu ya kila jambo wanalokusudia kulifanya. Hii huifanya saikolojia ya mwanamke kujenga kujiamini kwa kila jambo na hatimaye kufikia hatua za juu kabisa za maendeleo. Kumbe utegemezi kwa mume kwa kila kitu ni jambo ambalo linamfanya mwanamke asiheshimiwe ndani ya nyumba? Huu ndio uhalisia ulipo katika jamii kuhusiana na suala hili.

4.2.4 Kukosana Baina ya Wanandoa

Nyimbo za harusi za Zanzibar zimesheheni dhamira mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosana baina ya wanandoa ambao ni mke. Kukosana huko husababishwa na mambo mbalimbali za ndani na nje ya familia. Suala hili lina uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii ambapo tumeshuhudia kuwepo kwa taasisi za kushughulikia masuala haya zikiwepo na kufanya kazi yake vizuri. Miongoni mwa mambo ambayo yanasababisha wanandoa kutokuelewana na kukosana yale ya kukamatana ugoni na

kupishana mawazo juu ya vipaumbele katika familia. Mzee Juma Ali Bakar wa Bait Al Ras alitueleza kwamba:

> Miongoni mwa mambo ambayo yanasababisha wanandoa kutokuelewa baina yao ni kutofautiana katika kupanga vipaumbele katika maisha. Wengi kati ya wanawake katika ndoa hutaka mambo ya starehe na anasa badala ya kuwekeza katika mambo ya msingi kama kusomesha watoto pamoja kujenga nyumba. Utasikia kila mara bwana anapopata mshahara yeye anataka akanunue baibui, viatu, hereni, mkufu na manukato ya aina kwa aina. Gharama ya vitu hivi ukiitazama unaona kwamba ni kubwa kuliko hata mshahara wenyewe na hapa ndipo ugomvi unapoanzia. Kwa wale ambao wanakazi ya kuwaingizia kipato, mara nyingi fedha zao humalizia katika masuala hayo ya mambo ya anasa na tena kuomba zingine kutoka kwa waume zao (10/04/2017).

Nukuu hii inaonyesha kuwa kutokuelewana katika familia mara nyingi kunatokana na masuala ya fedha hasa pale mume na mke wanaposhindwa kukubaliana katika vipaumbele katika maisha yao. Inapotokea hali kama hii daima kutakuwa na mivurugano ambapo mke ataona kwamba hasikilizwi na hivyo mahitaji yake yanaonekana kuwa hayana maana yoyote. Mume naye humuoana mke kama mtu ambaye hana uoni wa maendeleo na hatimaye kumdharau jambo ambalo linafanya sasa waishi kwa chuki baina yao. Hili jambo halisi kabisa katika jamii ambapo kwa mujibu wa nadharia ya Saikolojia changanuzi mwanamke anapoona kuwa mahitaji yake yanaonekana kuwa hayana umuhimu anajiona kuwa ni mtu asiyekuwa na thamani yoyote na hivyo kujenga chuki dhidi ya mumewe jambo linalowafanya waishi maisha ya kutokuewana vizuri na kuwa na kauli moja katika masuala ya familia yao.

4.2.5 Imani za Kishirikina

Suala la imani za kishirikina lipo katika jamii na lina uhalisia usiokuwa na shaka ndani yake licha ya kuwa sisi kama wanataaluma hatuamini nguvu yake. Hii inatokana na ukweli kuwa, binadamu ni mtu ambaye kwa asili ni mtu mwenye wivu wa kutaka mambo mazuri yawe kwa upande wake tu na sio kwa watu wengine. Haya tunayaona katika shughuli za harusi ambapo watu wengine hawapendi kuona binti au kijana wa kiume anaoa na hivyo hujaribu kufanya mambo ya kishirikiana kwa lengo la kuwafanya wanandoa hao wasiweze kuishi pamoja. Tumeona nyimbo kadhaa za harusi zikiwasilisha dhamira hii na tulipotaka kufahamu kama katika jamii suala hili lipo ndipo tukaelezwa na Said Rashid Suleiman wa Chumbuni ya kwamba:

> Kufanyiana mambo ya kishirikina katika jamii ya Waswahili ni jambo la kawaida kabisa hususani katika masuala ya maendeleo. Mtu kuoa au kuolewa ni moja kati ya hatua kubwa ya maendeleo katika maisha yake. Lakini wapo baadhi ya watu ambao huwa hawapendi kuona jambo kama hilo linafanyika kwa sababu zao mbalimbali. Moja ya sababu kubwa ni roho mbaya tu ya kuona kwamba ni kwa nini fulani apate mafanikio hayo ya kuoa au kuolewa. Watu wa aina hii ni wabaya sana katika jamii na ni vizuri wakapewa elimu ili waachane na kazi hiyo (10/04/2017).

Kimsingi, nukuu hii inatuthibitishia kuwa katika jamii masuala ya imani za kishirikina yapo na yanachukuwa nafasi kubwa katika maisha ya watu. Kama mtu hapendi kuona mtu fulani akifanikiwa katika maisha, ni dhahiri kuwa mtu huyo atamia muda wake mwingi katika masuala ya kishirikina ili kuhakikisha kuwa huyo asiyetakiwa kupata maendeleo hayapati kabisa. Hata hivyo, kwa kuwa hili ni suala la imani na pale inapokuwa yule anayefanyiwa ushirikina haamini katika ushirikina hawezi kupatwa na tatizo lolote na daima ataendelea kupaa na kupata maendeleo ya juu kabisa. Wanasaikolojia changanuzi wanatoa ufafanuzi kuwa ushirikina ni suala la

kiimani ambapo mtu anapoiaminisha imani yake katika masuala ya saikolojia ndipo hapo yanampata matatizo chungu nzima. Hata inapokuwa ni tatizo la kawaida tu la kibinadamu atasema hapana hapa kuna mtu tu ambaye ndiye ananifanyia hivi. Hii itamfanya kutumia muda mwingi katika mambo hayo ikiwa ni pamoja na kwenda kwa waganga kulipiza kisasi kwa mambo ambayo hayana msingi wowote. Maendeleo hapa yanakuwa ni magumu kupatikana kwa sababu muda wa kufanya kazi unakuwa haupo. Hii ni jambo hatari ambalo kupitia elimu kwa umma linaweza kupungua kwa kiasi kikubwa katika jamii.

4.2.6 Uhalisia wa Uzuri wa Mwanamke

Suala la wanajamii kupenda kumuoa mwanamke kutokana na uzuri wake ni jambo halisia katika jamii. Vijana wengi wanapenda wanawake kutokana na uzuri wa sura yake hata kama kwa upande wa tabia hatajwi kwa uzuri. Tulifanya usaili na bwana Mansour Muhsin Swalehe ambaye alitueleza kuwa:

> Katika jamii yetu vijana wengi wanapenda kuoa mwanamke ambaye akipita naye barabarani watu watamsifu kwamba jamaa ana mke mzuri pengine kuliko vijana wote katika mtaa wao. Hili ndilo jambo linawafanya vijana kupenda kuoa wanawake wazuri wa sura na umbo na anaposifiwa yeye ndiye anasikia raha. Katika hali kama hii ni rahisi sana kupata mke ambaye hana maadili mazuri na mwishowe ndoa huvunjika mapema kabisa (12/04/2017).

Nukuu hii inadhibitisha kuwa ni kweli suala la vijana kupenda kuoa mwanamke ambaye ni mzuri wa sura ni suala la kawaida katika jamii ambapo mume hupata sifa kwa kuwa na mke mzuri. Kisaikolojia ni kawaida ya kila mtu kupenda kusifiwa kwa uzuri na hapa tunamuona mume akijisikia raha kutokana na kuwa na mke mwenye mvuto kwa kila anayemuona. Jambo la kujiuliza ni kuwa kuna faida gani ya mke wa

mtu kuanza kusifiwa na watu wengine kama sio njia ya watu hao kurudi baadaye na kuanza kumtaka mke huyo? Kwa mtu mwenye fikira nzuri na sahihi hawezi kufanya jambo kama hili bali ataoa mwanamke mwenye kusifika na kupambika kwa tabia nzuri.

4.2.7 Uhalisia wa Mapenzi

Nyimbo za harusi za Zanzibar zimesawiri dhamira ya mapenzi ambapo mke na mume wanaaswa kudumisha mapenzi baina yao ili kuifanya ndoa yao iweze kudumu miaka mingi zaidi. Katika maisha halisia ya jamii tumeona kuwa wapo badhi ya wanamume na hata wanawake ambao hawana mapenzi ya dhati kwa wenzi wao. Hii inatokea pale ambapo mume anachua uamuzi wa kumpiga mke wake tena wakati mwingine katika hadhara ya watu. Hiki ni kitendo kibaya ambacho ni kinyume kabisa na maadili ya jamii. Tulipozungumza na Ashura Mohamed Mwinjuma wa Mlandege kuhusiana na suala hili alitueleza kuwa:

> Mapenzi ya dhati siku hizi ni magumu sana kuyapata ingawa bado yapo kwa watu wachache sana ndani ya jamii yetu. Utaona mume anampiga mke wake mbele za watu na wakati mwingine hata nguo humvuka mkewe na watu kuona maungo yake ya siri. Kumpiga mke hadharani ni kitendo cha udhalilishaji ambacho kinafaa kupingwa kwa nguvu zote. Hivi juzi juzi katika mtaa wetu tulimuona bwana mmoja akimpiga mke wake bila ya huruma na ndipo tulipochukua hatua ya kwenda kuamulia. Hii yote inaonyesha kuwa mapenzi ya dhati katika jamii yamepotea na kutokana na wengi kupenda fedha na mali. Baadhi ya mabinti huvutiwa na wanamume kwa sababu tu ni watu wenye fedha bila hata ya kuchunguza tabia zao. Hii huwafanya kuolewa na watu ambao hawana huruma na hatimaye kuishia kupigwa (15/05/2017).

Nukuu hii inaashiria kwamba kukosekana kwa mapenzi ya dhati katika jamii kunachangiwa na fedha ambapo mwanamke anaweza kuvutiwa na mwanamume na kukubali kuolewa naye kwa sababu tu mwanamume huyo ni tajiri. Daima saikolojia ya binadamu humwelekeza katika kutamani fedha na mali na anapomuona mwanamume mwenye uwezo huo basi huvutiwa naye. Hii imewafanya wanawake wengi katika jamii yetu kujikuta wameolewa na watu ambao ni majambazi wasiokuwa na huruma wa aina yoyote ile. Watu hawa huwa ni kama wanyama katika matendo yao ambapo hakuna tendo hata moja ambalo wanalifanya kistaarabu.

4.2.8 Uhalisia katika Uwajibikaji

Uwajibikaji katika kutimiza majukumu ni kitu muhimu sana kwa kila mwanajamii katika kuhakikisha kuwa malengo yake yanakamilika. Tumeona katika nyimbo za harusi za Wanzanzibari kukihimizwa uwajibikaji kwa mume na mke kila mmoja katika nafasi yake ili kuhakikisha kuwa maisha ya familia yake yanakwenda vizuri. Suala hili lina uhalisia katika jamii ambapo tunawaona wanawake wakichakarika katika shughuli za maendeleo na kuachana na ile hali ya kukaa nyumbani kusubiri mume alete kila kitu. Wanawake wengi hivi sasa ndio wanaoongoza katika shughuli za ujasiriamali na kuchangia katika pato la familia na taifa kwa jumla. Pia, wapo akina mama ambao pamoja na kujishughulisha katika shughuli za ujasiriamali pia wanatimiza wajibu wao kama mama katika familia. Tulizungumza na Mzee Yusuf Mussa Sheikh wa Malindi akatueleza ya kwamba:

> Wanawake wa siku hizi tofauti sana na wale wa enzi zetu ambao kulingana na utamaduni wetu walikuwa ni watu wa kukaa nyumbani kusubiri kuletewa kila kitu na waume zao. Wanawake wa siku hizi wapo wengi katika utumishi wa umma na katika sekta binafsi kama wafanyakazi ambao wanapata mshahara na kuutumia katika kukuza ustawi wa familia zao. Hii ni kwa sababu wamepata fursa ya kupata elimu tofauti na wake zetu ambao walionekana kuwa ni watu wa ndani tu ambao walipewa elimu ya kuishi maisha ya ndoa tu lakini si katika shule kwa kiwango kama cha sasa ambapo wanawake wote wanapewa fursa ya kupata elimu na baadae fursa ya kuajiriwa na kujiajiri (23/05/2017).

Suala la uwajibikaji wa mwanamke katika jamii tunaliona likijitokeza katika dondoo hapo juu ambapo wanawake wanabainishwa kama watu ambao hivi sasa wameshika majukumu makubwa katika jamii na wanayamudu kisawasawa. Uwajibikaji huo tunauona pale wanaposadiana na waume zao katika kuwasomesha watoto wao. Huu ndio uwajibikaji ambao unatakiwa katika jamii ambapo mume na mke wakishirikiana kwa pamoja watasaidia katika kusukuma mbele maendeleo ya familia na taifa kwa jumla.

4.3 Hitimisho

Sura hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana na malengo mahususi mawili ambayo yalikuwa ni kuchambua dhamira na kisha kuelezea uhalisia wa dhamira za nyimbo za harusi ya jamii ya Wanzanzinari. Dhamira tulizoziwasilisha pamoja na suala la kupata watoto, suala la kutoka nje ya ndoa, kuheshimiana baina ya wanandoa, kukosana baina ya wanandoa, imani za kishirikina, uzuri wa mke, mapenzi katika nyimbo za harusi na uwajibikaji. Kwa ujumla tumefanikiwa kukamilisha malengo mahususi ya utafiti huu kwa mafanikio makubwa.

SURA YA TANO

HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.0 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni kuchambua dhamira katika nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Wazanzibar na kuelezea uhalisia wa dhamira hizo katika jamii ya leo ya watu wa Wazanzibar. Katika kutimiza malengo mahususi ya utafiti huu tumefanikiwa kuwasilisha jumla ya dhamira nane ambazo ni suala la kupata watoto, suala la kutoka nje ya ndoa, kuheshimiana baina ya wanandoa, kukosana kwa wanandoa, imani za kishirikina, uzuri waa mwanamke, mapenzi na uwajibikaji.

Dhamira inayohusu wanandoa kupata watoto mara baada ya kuona imeonekana kujitokeza katika nyimbo za harusi zilizotafitiwa na kubainika kuwa ni suala la jamii nzima na si wanandoa peke yao. Vijana wa rika wanapooana hutarajiwa kupata watoto muda mfupi wanapoanza maisha yao ya ndoa. Tumebaini kuwa inapotokea kukawa na ugumu wa kupata mtoto saikolojia ya mke na mume huathirika kiasi cha kuchukua maamuzi ambayo ni hatari kwa maisha yao. Jambo la msingi la kujifunza hapa ni kwamba zipo sababu nyingi ambazo zinaweza kuchangia wanandoa kutopata mtoto kwa haraka kama wao wenyewe walivyopanga na kutaraji. Hivyo, itakuwa ni busara kwao kuchukua hatua muafaka za kutatua tatizo ili mambo yao yawe vizuri. Katika uhalisia wa maisha ya kila siku wapo wanandoa wengi ambao hukumbwa na hali kama hii na hukua hatua stahiki katika kukabiliana na hali hiyo.

Dhamira ya wanandoa kutoka nje ya ndoa na kuwa na mahusiano ya kingono na watu wengine imejitokeza katika nyimbo za harusi tulizozitafiti. Kitendo hiki ni

kibaya kwani huleta madhara makubwa katika familia hususani katika kipindi hiki cha utandawazi ambapo kuna mfumuko wa magonjwa. Imebainika kuwa wanamume ndio ambao wanapenda kuwa na mahusiano na watoto wadogo wa kike huku wakiwaacha wake zao ndani. Hii inaonyesha ni kwa kiwango gani wanajamii wanavyokuwa na utovu wa nidhamu kwani kufanya hivyo si tu kwamba ni kinyume na maadili ya jamii bali pia kinyume na maadili ya dini. Watu wa aina hii hujidanganya kuwa kwa kufanya hivyo watapata starehe zaidi kuliko ile wanayoipata wanapokutana na wake zao kimwili. Huku ni kujidanganya tu na kujiongezea matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuhudumia mwanamke zaidi ya mmoja kimaisha hali ya kuwa kipato cha wanamume wengi wa aina hiyo ni kidogo kisichoweza kukidhi mahitaji ya familia yake.

Suala la kuheshina baina ya wanandoa nalo limesawiriwa katika nyimbo teule ambapo tumeona kwamba mke na mume wanashauriwa kuheshimiana baina yao kwani ndilo jambo la msingi ambalo litawafanya waishi maisha yao kwa amani, furaha na upendo. Imetokea mara nyingi katika jamii kuona baadhi ya wanandoa wakiishi bila kuheshimiana na kusababisha wao kusemana vibaya hata mbele za watu. Suala kama hili halikubaliki kwani hutoa mafunzo mabaya kwa watoto na watu wengine katika jamii. Mke na mume wanapoheshimiana hata mapenzi baina yao nayo hukua zaidi.

Kukosana baina ya mke na mume ni jambo la kawaida kama ilivyo kwa watu wengine katika jamii ambao nao huwa wanakosana na kupatana pia. Mara nyingi watu wawili wanapoamua kuishi pamoja huku kila mmoja akiwa na tabia tofauti na ya mwenzake kulingana na malezi aliyoyapata kutoka kwa wazazi wake ni lazima

watakosana. Hivyo, kukosana ni jambo la kawaida na jambo la msingi sasa ni wao kukaa pamoja na kutazama ni nini kilichowakosanisha na kupata ufumbuzi wake na hatimaye kuishi kwa amani na upendo. Katika maisha halisia ya jamii tumeshuhudia mke na mume wakikosana tena kwa ugomvi mkubwa lakini mara baada ya muda mfupi na wakati mwingine muda mrefu hujishuluhisha na kumaliza tofauti zao.

Suala la imani za kishirikina nalo tumeliona likijitokeza katika nyimbo zilizoteuliwa ambapo tumeona bibi harusi akitahadharishwa na washirikina. Washirikina wanatajwa kuwa hawakupenda kuona bibi harusi anaolewa na hivyo wataendelea na ushirikina wao ili kumdhuru huko huko kwa mumewe. Ushirikina katika jamii ni kitu ambacho kipo kila siku na ni suala la imani tu ambapo kama mtu haamini katika imani hizo kamwe hawezi kupata matatizo yoyote. Jamii inaaswa kutoendekeza imani za kishirikina kwa sababu hazina tija yoyote ile.

5.1 Hitimisho

Kwa jumla, matokeo ya jutafiti yamebainisha kuwa nyimbo za harusi za jamii ya watu wa Zanzibar zina zinaeleza masuala muhimu katika maisha ya binadamu. Nyimbo hizi zinatazamwa kama chombo cha kuijenga jamii kimaadili ili iweze kuishi katika ustawi mzuri wenye muafaka. Katika usaili tulioufanya na baadhi ya watafiti tumeweza kubaini kuwa wanajamii wanazidhamini sana nyimbo zinazoimbwa katika harusi. Nyimbo nyingi zinakuwa zimewasilishwa kwa kutumia lugha ya mafumbo ambayo kwa watu wazima inatajwa kuwa wanaweza kuelewa maana yake. Wazazi wa binti anayeolewa na wale wa yule ambaye anaoa huwa wanakuwa na matarajio makubwa sana juu ya ustawi wa familia za watoto hao na hata siku moja hawapendi kuona wakipata matatizo.

5.2 Mapendekezo

Baada ya kukamilika kwa utafiti huu tunapendekeza kwamba utafiti kama huu unaweza kufanywa katika jamii nyingine mbalimbali za Tanzania ili kuona ni kwa vipi nyimbo za harusi zinaweza kuwa ni chombo muafaka cha kufunza masuala mbalimbali muhimu katika maisha ya jamii.

Pia, tunapendekeza utafiti kama huu ufanyike katika jamii mbalimbali za Zanzibar ambazo zinaishi katika ukanda wa kaskazini na kusini. Mathalani, utafiti unaweza kufanywa katika maeneo ya Watumbatu, Makunduchi na Wete na Chakechake kisiwani Pemba.

MAREJELEO

Ali, M. (2014). “Taashira na Utendaji katika Nyimbo za Harusi za Waswahili Kisiwani Unguja.” Tasinifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Babbie, E., (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Beyanga, A. (2016). “Taswira ya Ng’ombe katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Washubi,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Bouman, Z. (2003). *Liquid Love: On the Frailty of Human Bonds*. Cambridge: Polity Press.

Chapman, H. M. (2011). *Love: A Biological, Psychological and Phisiological Study*. Rode Island: University of Rode Island Press.

Creswell, J.W. (2009). *Research Design: Qualitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Duck, S. (2007). *Human Relationships*. London: Sage Publication.

Fakih, B. A. (2017), “Kuchunguza Dhamira Dhati ndani ya Nyimbo za Bongo Fleva,” Tasinifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Khalifa, A.S. (2013). “Usawiri wa Kijinsia katika Nyimbo za Bongo Fleva,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Kirumbi, P. S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Kombo, D.K. and D. L. Tromp (2006). *Proposal and Thesis writing and Instroduction.* Africa Nairobi: Paulines Publications.

Kumar, R., (1999). Research *Methodology A step-by guide for beginners*. New Delhi: SAGE Publication.

Kothari, C. R. (2008). *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques* New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Matteru, J. (1983). "Fasihi Simulizi na Uandishi." katika Makala ya Semina ya Waandishi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mungai, M. J. (2014). "Fani katika Nyimbo Teule za Anastacia Mukabwa." Tasinifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu na Chimerah, C. (1999). *Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: JKF

Omari, S. (2009). "Tanzania Hip Hop As Popular Literature, "Unpublished *Ph.D Thesis*. UDSM.

Omary, M. (2015), "Kuchunguza Ufasihi Simulizi katika Kazi za Euphrase Kezilahabi: Mfano wa Vitabu vya *Kichomi*, *Karibu Ndani* na *Dhifa*," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ramadhani, S. K. (2013). “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee”. Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Robson, C. (2007). *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Samwel, M. (2010). Masuala ya Kisiasa katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo Fleva, katika *Mulika* namba 18. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Sengo, T. S. Y. (1985). Folkes from Pemba and Unguja, University of Khartoum, Sudan.

Sengo, T. S. Y. M. (1987). *Fasihi Simulizi*, *Sekondari na Vyuo*: Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.

Sengo, T. S. Y. (1992). “Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja.” Katika Nordic Journal of African Studies.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA.

Sengo, T. S. Y. M. na Kiango, S. D. (2012). *Hisiya Zetu*, Dar es Salaam: TUKI.

Sherwood, L. (2006). *Fundamentals of Physiology: A Human Perspective*. Belmont: Thomson Books.

Smart, C. (2007). *Personal Life*. Cambridge: Polity Press.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Yalwala, P. (1991). "Maudhui katika Nyimbo za John Mwale." Tasinifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Yin, R. K. (1994), *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V. (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

VIAMBATANISHI

KIAMBATANISHI A : MASWALI YA USAILI KWA WAZAZI

Ndugu muhusika

Utafiti huu unahusisha mada ya Kuchunguza Lugha ya Mafumbo katika nyimbo za harusi, Wilaya ya Mjini Unguja. Lengo ni kukusanya taarifa zitakazosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Mchango wako nitauthamini na kuuamini na majibu ya maswali ni kwa ajili ya utafiti huu na si kwa lengo jingine lolote. Hivyo utakuwa ni siri na ni wa manufaa kwa ajili ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Utafiti huu utasaidia kuwa chachu ya kuendeleza mila, na desturi za jamii.

Hivyo basi nakuomba mashirikiano mazuri katika kujibu maswali yafuatayo hapa chini.

Natanguliza shukrani zangu za dhati.

1. Jinsi: Mke ☐ Mume ☐

Umri: Miaka ☐

Umeolea/hujaolewa..... Umeoa/hujaowa.....

Mjane (Kufiwa/Talaka).....

Kazi yako: (mf.Mwalimu, Mkulima).....

Namba ya Simu..... Kiwango cha elimu ……

Umezaliwa wapi? Kijiji..... Shehia.....

Mji.....

2. Ainisha nyimbo tatu zinazoimbwa katika harusi za Wazanzibari.

3. Nyimbo zote zinazohusiana na harusi hupatikana wakati gani?

i. Siku ya singo

ii. Siku ya ndoa ☐

iii. Baada ya ndoa ☐

4. Elezea dhamira zinazopatikana katika nyimbo za harusi ulizozitaja.

5. Eleza mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za harusi.

6. Elezea uhalisia wa dhamira za nyimbo za Harusi za jamii ya Wazanzibari.

7. Elezea jambo lolote muhimu ambalo sikuuliza katika mahojiano yetu.

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

KIAMBATANISHI B: MASWALI YA USAILI KWA

WATUNZI/WAIMBAJI WA NYIMBO ZA HARUSI

Ndugu muhusika

Utafiti huu unahusisha mada ya Kuchunguza Lugha ya Mafumbo katika nyimbo za harusi, Wilaya ya Mjini Unguja. Lengo ni kukusanya taarifa zitakazosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Mchango wako nitauthamini na kuuamini na majibu ya maswali ni kwa ajili ya utafiti huu na si kwa lengo jingine lolote. Hivyo utakuwa ni siri na ni wa manufaa kwa ajili ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Utafiti huu utasaidia kuwa chachu ya kuendeleza mila, na desturi za jamii.

Hivyo basi nakuomba mashirikiano mazuri katika kujibu maswali yafuatayo hapa chini.

Natanguliza shukrani zangu za dhati.

1. . Jinsi: Mke ☐ Mume ☐

Umri: Miaka ☐

Umeolea/hujaolewa..... Umeoa/hujaowa.....

Mjane (Kufiwa/Talaka).....

Kazi yako: (mf.Mwalimu, Mkulima).....

Namba ya Simu.....Kiwango cha elimu ……

Umezaliwa wapi? Kijiji..... Shehia.....

Mji.....

2. Naomba unitajie nyimbo za harusi ambazo umewahi kuzitunga wewe binafsi.
3. Ni mambo gani yanayokusukuma kuandika/kutunga nyimbo za harusi?
4. Nyimbo zako zina dhamira gani?
5. Ni upi mwitiko wa jamii ya leo kwa nyimbo za harusi ukilinganisha na ilivyokuwa kwa jamii za miaka ya nyuma?
6. Eleza uhalisia wa dhamira za nyimbo zako kwa jamii ya leo ya Wazanzibari wa Kisiwani Unguja.
7. Eleza jambo jingine lolote muhimu kuhusiana na utunzi wako wa nyimbo za harusi ambalo sijakuuliza na unadhani ni muhimu mimi kulifahamu.

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO

KIAMBATANISHI C: MASWALI YA USAILI KWA WANANDOA WAKATI WA HARUSI KUTOKANA NA NYIMBO ZA HARUSI ZIIMBWAZO WAKATI HUO

Ndugu muhusika

Utafiti huu unahusisha mada ya Kuchunguza Lugha ya Mafumbo katika nyimbo za harusi, Wilaya ya Mjini Unguja. Lengo ni kukusanya taarifa zitakazosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Mchango wako nitauthamini na kuuamini na majibu ya maswali ni kwa ajili ya utafiti huu na si kwa lengo jingine lolote. Hivyo utakuwa ni siri na ni wa manufaa kwa ajili ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Utafiti huu utasaidia kuwa chachu ya kuendeleza mila, na desturi za jamii.

Hivyo basi nakuomba mashirikiano mazuri katika kujibu maswali yafuatayo hapa chini.

Natanguliza shukrani zangu za dhati.

1. Jinsi: Mke ☐ Mume ☐

Umri: Miaka ☐

Umeolea/hujaolewa..... Umeoa/hujaowa.....

Mjane (Kufiwa/Talaka).....

Kazi yako: (mf.Mwalimu, Mkulima).....

Namba ya Simu..... Kiwango cha elimu ……

Umezaliwa wapi? Kijiji..... Shehia.....

Mji.....

2. 2.Ainisha nyimbo tatu zinazoimbwa katika harusi za Wazanzibari.
3. Elezea dhamira zinazopatikana katika nyimbo za harusi za Wanzibari.
4. Eleza mafunzo yanayopatikana kutokana katika nyimbo za harusi za Wanzibari.
5. Nyimbo za Harusi za Wazanzibari zinakufunza nini wewe kama mwanandoa?
6. Nyimbo za harusi za jamii ya Wazanzibari zina uhalisia wowote kwa jamii?

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO

KIAMBATANISHI E: Nyimbo za Harusi

1. Iyoo, kawaida ya harusi iyooo

Iyoo, kawaida ya harusi iyooo, Iyooo

Salamaeee yalla salamaaa, Ishallaa salmini

Salmina akbaru shoo, Shoo

Salmina akbaru, takabalmina, maliki yaumidaa Allahu akbar

Wayusali Wasalam

Wayusali Wasalam

Vigelegele kidogo.

2. Naiwe leo aee

Naiwe leo aee Naiwe leo furaha

Bibi amepeta bwana Naiwe leo furaha

Bwana amepeta bibi Naiwe leo furaha

Mtango nautambae Naiwe leo furaha

Wende ndani ukazae Naiwe leo furaha

Wazae mke na ndume Naiwe leo furaha

Waje hapa tuwatume Naiwe leo furaha.3.

3. Alosema haolewi

Alosema haolewi, mbona kaolewa x2

Alosema hampati, mbona kampata x2

Alosema hayawi, mbona yamekuwa x2

Mbona yamekuwa, we hoya, mbona yamekuwa

4. Viti viwili mfano

Viti viwili mfano, matendegu sawasawa

Viti viwili mfano, matendegu sawa

Matendegu sawasawa, hoya, matendegu sawasawa.

5. Alosema haolewi

Alosema haolewi, herine anazovishwa si za bure

Mwambieni mwari wenu asikie viatu, anavyovishwa si vya bure

Mwambieni mwari wenu asikie na shanga, anazovishwa si za bure

Mwambieni mwari wenu asikie na kanzu, anayovishwa si ya bure

Mwambieni mwari wenu asikie na pete, anayovishwa si ya bure.

6. Babu Juma kuchukuyu nini

Babu Juma kuchukuyu nini, kombe na vidagara

Humo mkobani muna nini, Rungu lina garagara

7. Kuna ila moja ila yako dada ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Kutwa kwenda kwa mama ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Kitanda hutandiki ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Na mamiyo kanayo ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Leo nimechoka ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Mume umwite bwana ila

Kuna ila moja ila yako dada ila, Kulala na chupi ila.

8. Kuna ila moja ila

Kuna ila moja ila yako bwana ila, Kigongo mkononi ila

Kuna ila moja ila yako bwana ila, Mke kumwita bibi ila

Kuna ila moja ila yako bwana il, Kula mkahawani ila

Kuna ila moja ila yako bwana ila, Kufanya na damu ila.

9. Raruwa dereva raruwa,

Raruwa dereva raruwa, Umeyataka kwa hiari yako

Utaupanda mlima, Utaupanda mlima

Mlima una mawe uwoo, Utaupanda mlima

Mlima una ndago uwoo, Utaupanda mlima

Mlima wateleza uwoo, Utaupanda mlima

Hauna vishindo uwoo, Utaupanda mlima.

10. Halina mana we halina mana we

Halina mana we halina mana we, Halina mana ntalikata x2

Lawezangu linafuliwa pete, langu mie liko teketeke

Halina mana ntalikata halina mana we, halina mana we halina mana ntalikata

Lawenzangu linatoa matunda, langu mie linatoa mafunza

Halina mana ntalikata halina mana we, halina mana we halina mana ntalikata

Lawenzangu linatoa maraha, Langu mie linaninyima raha

Halina mana ntalikata halina mana we, halina mana we halina mana ntalikata

11. Tunao mti tunao

Tunao mti tunao, twende nao polepole, x2

Tukaupasuwe mbao, mashina hadi vilele.

Ndege inapita juu inakimbia michanga x2

Bwana konda nisubiri , nimezisahau shanga

Kuteta watete wao miye ninawatazama,

Kuja nikiteta miye hunishushia lawama,

Mwaka huu mwaka wao, kutota au kuzama.

Bwana huyu madhubuti, wanawake ishirini,

Kumi kawaweka shamba kumikaweka mjini,

Lingelikuwa shoka bovo lingekatika mpini.

12. kutandika kuna maanae

Ukitaka mume akae, kutandika kuna maanae

Ukitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi

Ukitaka mume adumu, kutandika kuna maalumu

Ukitaka mume asilale, kutwa moto kwenye kigae.

13. Nalilia pembe langu

Nalilia pembe langu

Pembe nipewa ni mama pembe, Nalilia pembe langu

Pembe nipewa ni baba pembe, Nalilia pembe langu

Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi

Nalilia pembe langu.

14. Hongera mwanangu wee hongera

Hongera mwanangu wee hongera na mimi mamayo we nihongere

Mama uchungu mama uchungu, nyamara mwanangu hoyee,

Nyamara mwanangu tumbo la udere, linauma mnowe hoya,

Linauma mnowe, hoya linaumawe oya.

15. Mtaimbo wa Kizungu

Mwanangu lia wee, Mtaimbo wa kizungu hauna sharia x2

Mwanangu cheka wee, Mtaimbo wa kizungu haulala weka x2

Mwanangu udumbe wee, Mtaimbo wa kizungu kazi yake punde x2

16. Nyang'anya nyang'anya

Nyang'anya nyang'anya, Mnyang'anya hunyang'wa,

kaanza yeye kunyang'anya

Kaanza yeye kunyang'anya, Kaanza yeye kunyang'anya.

17. Tumempata hatuja mpata

Tumempata hatuja mpata, Tumempata mweupe kama mmanga

Tumempata hatuja mpata, Tumempata mweupe kama mmanga.

18. Hodi wee hodi ya mwana mirambo,

Hodi wee hodi ya mwana mirambo,

umetwitwa tumekuja, mgeni havunji kiambo

Umetwitwa tumekuja, mgeni havunji kiambo.

19. Sheti upembejele,

sheti upembejele x2

Mwanamme cheche ya moto, sheti upembejele.

20. Kungwi mwambie mwari wako

Kungwi mwambie mwari wako, asiache ufunguo,

akiacha ufunguo, watafungua wenziwe.

Kungwi mwambie mwari wako asiache kujipamba,

Asipojipamba, watajipamba wenziwe.

Kungwi mwambie mwari wako amsinge mumewe,

Asipomsinga, atasingwa na wenziwe.

21. Leo nileo ooo, leo ni leo ooo

Leo nileo ooo, leo ni leo ooo, utauona mpambano kweli si uongo

Jamani harusi mtoto wa watu, jamani harusi mtoto wa watu

Tumemzingua, kwa yasini tatu, jumemzingu kwa yasini tatu

Asijedhurika, asijedhurika kwa macho ya watu, leo ni leo ee

22. Masomaso we mwanangu usimuone

Masomaso we mwanangu usimuone,

Masomaso we mwanangu usimune,

Kwa jicho la hasidi we mwanangu usimuone,

Masomaso we mwanangu usimuone,

Maso, mwanangu usimuone, maso, mwanangu usimuone.

23. Bwan-Juma mbona kunlala

Bwan-Juma mbona kunlala selala nautia kasi

Kwa mapana kama kibiriti,

Kwa marefu kama boriti,

Hebu tia kama haupiti.

24. Watoto lala

Watoto lala natakamkomoa baba yenu,

Nikimpa robo ananuna,

Nikimpa nusu ananuna,

Natakampa yote nyama.

25. Watoto muwaa

Watoto muwaa watoto mua, haunyonywa ulala

Watoto mua kifundo mwakijua, haunyonywa ulala

Watoto mua ukila wasinzia, haunyonywa ulala

Watoto mua ukila wazimia, haunyonywa ulala

Usiku wa jana seupata vyema mua, haunyonywa ulala

Ukimuona mwambie aje tena mua, haunyonywa ulala

Huo mua haunyonywa ulala, huo mua haunyonywa ulala

26. Haulala

Haulala uwooo, haulala, una maradhi gani

Ukilala walalia pajani haulala, unamaradhi gani

Ukila walalia mamboni haulala, unamaradhi gani

27. Kinanichomaaa kinanichoma

Kinanichomaaa kinanichoma, kijiti cha mpera

Wapi? Hapa, patie dawa sana, pasije pakabana,

Pakamkera bwana,wakati wa kulala,Usiku na mchana.

28. Twende dereva twende

Twende dereva twende twende wee,

Mungu atatujalia salama twendedereva twende,

Mwabie dereva we asende mbio, usiku twangojwa we sie wenzio

Usikutwangojwa we, sio wenzio usiku twangojwa we sio wenzio

Mwambie dereva kidogo kidogo, atalichezea we shina la muhogo

Atalichezea we, shina la muhogo, atalichezea we shina la muhogo

Mwambie dereva we asirudi nyuma, asiku angojwa we achezee nyama, Usiku angojwa We achezee nyama, usiku angojwa we achezee nyama

29. Hodi hodi

Hodi hodi mgeni haoni haya, hodi hodi mgeni haoni haya

Hodi, mgeni haoni haya, hodi, mgeni haoni haya.

30. Mwari angie chooni

Mwari angie chooni,

Kwa maulidi tukamkoshe marashi uvumba na udi x2

Uvumba na udi we, hoya, uvumba na udi.

31. Sonyombe sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

mume huitwa bwana, mwari we sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

Mume hupokewa, mwari we sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

Mume husingwa, mwari we sonyombe

Sonyombe, sonyombe, mwari we sonyombe

Mume hukogeshwa, mwari we sonyombe

32. Kero kero

Kero keero we, kero kero we, kero kila siku

Kwenda kwa wazazi we kero kero

Uinamie chini we, uinamie chini x2

Unapokwenda nyumbani kwa watu, uinamie chini.

33. Mchi Kibete

Mchi kibete weee, mchi kibete ndiwo utwangao

Mchi kibete weee, mchi kibete ndiwo utwangao

Ukitwanga watwangia matao, mchi kibete, ndiwo utwangao

Ukilala walalia pajani mchi kibete, ndiwo utwangao

Ukilala walalia tunduni, mchi kibete, ndiwo utwangao

34. Waitwa we Juma usikatae

Waitwa we Juma usikatae, ukawalishe ndege na wanawe x2

Waitwa we Juma usikatae, ukawarushie ndege na wanawe

Nahangaika, kila kukicha nahangaika mie kwa weye

Nahangaika, kila ukiona nahangaika mie kwa weye

35. Ukampare samaki

Umetaka kuolewa, Ukampare samaki

Samaki ana magamba, Ukampare samaki

Samaki ana mwiba, Ukampare samaki

Samaki ana matumba, Ukampare samaki